*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo




## Sven kumrithi Mr. Objective

Uk. 24

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00037 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Novemba 8 - 14, 2023 |

**KIMATAIFA**

Uk. 19



## Netanyahu: Israel itakuwa na jukumu la usalama Gaza



## Zitto alivyo sahihi kutosusia chaguzi

Uk. 8



**KOLAMU**

Uk. 17

## Mambo ambayo watu wenye nguvu ya akili hawayafanyi

Uk. 16

## Zijue sheria za kodi

# Marekani yamfagilia Samia

- **Yaahidi kufanya mambo makubwa sekta ya afya**

Uk. 4

**Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha huduma za afya, hasa katika huduma jumuishi kwa waathirika wa dawa za kulevya na VVU.**



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe (aliyesimama), akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, wakati akiongoza ujumbe wa wageni ukiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Msaidizi (PDAS) na Kaimu Naibu Mratibu Mkuu wa masuala ya Ukimwi wa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi (PEPFAR), Dk. Rebecca Bunnell, ulipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba na Kituo cha Warahibu wa Dawa za Kulevya cha jijini humo jana. Picha: Mpigapicha Wetu



## ... Wafanyabiashara wampongeza kufungua milango ya majadiliano

Uk. 4



## Rais IPU ajipanga kutoa tamko vita Mashariki ya Kati

Uk. 5

## Apollo ya India kujenga hospitali kubwa Dar

Uk. 2



## Makonda ziarani Mwanza siku tatu

# Makonda ziarani Mwanza siku 3

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

KATIBU wa NEC, Siasa, Itikadi na Uenezi Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu, Paul Makonda, anatarajia kuanza ziara ya kikazi ya siku tatu mkoani Mwanza kuanzia Novemba 11 hadi 13, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Katibu wa Itikadi na Uenezi, Mkoa wa Mwanza, Prudence Sempa, alisema wananchi wajitokeze kwenda kumsikiliza na kutoa kero mbalimbali.


Alisema Makonda anatarajia kuanzia ziara yake Wilaya ya Sengerema na atakagua mradi wa ujenzi wa daraja la Magufuli Busisi na atapokea taarifa ya serikali kuhusu maendeleo ya mradi huo.

"Wananchi wa Mwanza wanamsubiri na wote wenye kero mbalimbali wafike kumsikiliza na kwamba atapata fursa nzuri ya kuwasikiliza watu wa Mwanza.

"Mkumbuke kuwa Makonda ni jembe na mtoto wa Mwanza anapokuwa anazungumza na watoto wa Mwanza wenzake…Misungwi kutakuwa na tukio la kumpa uchifu, utaratibu wote utatekelezwa kama tulivyopanga," alisema Sempa.

Alisema Novemba 13, atakwenda Kisesa Magu na atazungumza na wananchi na baadaye tutamsindikiza kwenda Mkoa wa Simiyu kuendelea na ziara yake.

**Mkumbuke kuwa Makonda ni jembe na mtoto wa Mwanza anapokuwa anazungumza na watoto wa Mwanza wenzake… Misungwi kutakuwa na tukio la kumpa uchifu, utaratibu wote...**



Katibu wa NEC, Siasa Itikadi na Uenezi CCM, Paul Makonda

# Apollo kujenga hospitali kubwa Dar

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Kituo cha Umahiri na Ubobezi wa Kimatibabu 'Apollo Hospitali' kilichopo nchini India, umeanza kutathmini eneo itakapojenga Hospitali jijini Dar es Salaam. Uwekezaji huo utaleta chachu katika sekta ya afya.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, wakati wa mazungumzo na Rais wa Apollo Group Hospitals, Dk. K Hari Prasad, kilichofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema, majadiliano hayo yamefuatia kati ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia na uongozi wa hhospitali hiyo yaliyofanyika Oktoba 11, mwaka huu ambapo hadi sasa ni siku 27 tu zimepita tangu majadiliano hayo yafanyike.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Aidha,, Dk. Jingu allisema ndani ya miaka mitatu, hospitali hiyo itakuwa imeshajengwa na kuanza kufanya kazi.

"Tuna kila sababu ya kumshukukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona jambo hili ni muhimu ambapo uwekezaji huo utazidi kuboresha huduma za afya," aalisema.. Dk. Jingu alisema hatua hiyo ni katika kuhakikisha Tanzania inakuwa na kituo cha umahiri ukanda wa Kusini mwa Afrika, lakini pia ukanda wa Afrika Mashariki ambapo Tanzania imewekeza katika kuboresha huduma za afya hivyo kituo hicho cha umahiri, kitaongeza utalii wa matibabu na watu wengi watakuja kupata huduma za afya nchini," alifafanua Dk. Jingu Kwa upande wake, Rais wa Apollo Group Hospitals, Dk. K Hari Prasad, wakati akizungumzia mchakato unaoendelea baada ya kikao cha siku tatu kati ya hospitali hiyo na

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya,

alisema wamekuja Tanzania kuanzisha kituo cha matibabu bobezi ili kuongeza ubora wa huduma za afya nchini.

"Sisi tunaziba pengo lililopo na hatuji kwa sababu ya mashindano na watoa huduma wengine, tunaamini katika hili na ujio wa Bima ya Afya kwa Wote, pia utasaidia watu kupata huduma bora zaidi Tanzania na Bara la Afrika," alisema Dk. Prasad.

Alisisitiza namna watakavyosaidia kuleta huduma za kibingwa nchini ikiwemo matibabu kwa watoto wenye matatizo ya moyo na hasa yale magonjwa ambayo bado Watanzania wanafuata huduma hizo nchini India. "Tulisaini makubaliano kati ya Tanzania na India, tumekaa hapa kwa siku tatu, tumeangalia sera zilizopo na kuona eneo ambalo tutawekeza, tumefurahi sana na tunaamini miaka miwili ijayo, tutaanzisha huduma kwani tuna shauku na hatuna wasiwasi kuwekeza Tanzania," alisema Dk. Prasad.

Naye Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu, alisema wamekaa na uongozi wa Apollo kwa siku tatu na kufanya makubaliano kadhaa ikiwemo eneo ambalo hospitali hiyo itajengwa.

# RC Mtaka awa mbogo, awatolea uvivu wazazi

**Na Mwandishi Wetu, Njombe**

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amesema atawahamisha mkoani humo, wazazi watakaowazuia watoto waliofaulu kuendelea na masomo ya sekondari.

Amesema mzazi atakayemzuia au kugoma kumpeleka mtoto wake atakayefaulu kuendelea na masomo ya sekondari, atahama mkoa huo.

"Sitaki mchezo katika suala la elimu," alisema na kuongeza, "hataki kusikia mzazi kagoma kumpeleka shule mtoto katika Mkoa wa Njombe… hatua kali zitachukuliwa kwa atakayekaidi kumwendeleza mtoto wake."



RC Njombe, Anthony Mtaka

Alisema hayo Wakai akizungumza katika Shule ya Sekondari Mabatini, Mtaka alisema anawatakiwa heri wanafunzi wanaotarajia kuanza mtihani wa kidato cha nne hivi karibuni.

"Ninawataki heri wanafunzi wote mnaotarajia kuanza mitihani ya kumaliza kidato cha nne, " alisema.

Alisema mitihani ya kidato cha nne inatarajia kuanza Novemba 13, mwaka huu, hivyo kila mzazi azingatie kauli yake na kwamba atakayegoma atambue anahama Njombe.

Aidha, aliwataka wazazi kuwapunguzia majukumu wanafunzi ili waweze kujiandaa na mitihani ya taifa ya kidato cha nne ikiwamo kutumia muda mwingi kujisomea katika dakika za mwisho.

# Kambi kupandikiza nyonga, magoti bandia Mlongazila

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kwa kushirikiana na Hospitali ya Queen Elizabeth ya Uingereza, itafanya kambi maalumu ya upasuaji wa kuweka nyonga na magoti bandia kwa wagonjwa wenye changamoto za maradhi ya nyonga na magoti kuanzia Novemba 27 hadi Desemba mosi, mwaka huu.

Akielezea kambi hiyo, Daktari Bingwa wa upasuaji mifupa, nyonga na magoti, Shilekirwa Makira, alisema wagonjwa watakaonufaika na huduma hizo ni pamoja na wenye matatizo ya nyonga zilizosagika, zenye maumivu makali na magoti yaliyosagika.

Aliongeza watu wenye changamoto hizo watabadilishiwa kwa kuwekewa nyonga na magoti bandia kitu kitakachowafanya waondokane na maumivu wanayoyapata kabla ya nyonga zao kubadilishwa.



# Sekta rasmi, binafsi kujumuishwa kukuza uchumi

**Na Suleiman Rashid Omar, Zanzibar**

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zitaendelea kuwekeza katika kujenga mazingira wezeshi ili kuwa na uchumi imara unaojumuisha sekta rasmi na zisizo rasmi nchini.

Rais wa Zanzibar ambaye pi ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo katika hutuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, katika hafla ya ufunguzi wa Kongamano la Pili la Kimataifa la Usimamizi wa Biashara na Maendeleo ya Uchumi lililofanyika mjini hapa.

Alisema ili kuweza kuwa na uchumi imara Serikali zote mbili zinafanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu mbali mbali ikiwemo ujenzi wa barabara, reli, madaraja ya kisasa, bandari na viwanja vya ndege pamoja na miundombinu mengine ambayo ni nguzo muhimu katika kukuza biashara.

Rais Dk. Mwinyi alisema nchi haiwezi kuendelea kwa kutegemea ubunifu unaotoka mataifa yaliyoendelea katika ulimwengu wa sasa wenye ushindani wa kibiashara hivyo ni lazima tuwekeze na kuzitumia tafiti katika kutatua chamgamoto zinazoikabili jamii.

Alisema serikali zinaendelea kufanya juhudi za kukabiliana na changamoto ya ukuaji wa uchumi hasa katika kuhakikisha sekta binafsi inakuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kuwataka watafiti kufanya tafiti ambazo zitaonesha namna bora ya kuboresha mazingira ya biashara na kutoa ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na wananchi.

Rais Dk. Mwinyi alisema kasi ya ukuaji wa uchumi ni wastani wa asilimia 5.2 katika robo tatu ya kwanza ya mwaka 2022 kwa Tanzania Bara na 5. 4 kwa upande wa Zanzibar kulikotokana na jitihada za kuimarisha uchumi wa buluu, kuimarika kwa shuhuli za utalii na sera madhubuti za fedha na kibajeti.

Aliwataka wanataaluma na watafiti kulitumia kongamano hilo katika kubadilishana uzoefu na watafiti wa nchi za nje ili kuchota uzoefu na ujuzi ambao utakuja na suluhisho endelevu kwa changamoto zetu na kuepusha kuendelea kutumia tafiti za nje ambazo nyingi siyo sahihi kwa mazingira, teknolojia na historia ya nchi yetu.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, aliipongeza Wizara ya Fedha ya Tanzania kwa uamuzi wa kongamono hilo kufanyika Zanzibar ambalo litatoa fursa kwa washiriki kubadilishana uzoefu katika usimamizi wa fedha, kufanya tafiti zenye ubunifu na kutafakari namna ya kukuza uchumi wa nchi na taifa kwa ujumla.

Alisema Zanzibar imeanzisha Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi, Wasimamizi na Washauri wa Kodi (ZIATC) ambapo ameitaka Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) kujenga ushirikiano na Taasisi ya ZIATC ili kukuza na kuimarisha Uchumi wa Taifa.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa William Pallangyo alisema kupitia kongamano hili kutaibua mbinu mbalimbali kutoka kwa wataalamu wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.

Alisema uchumi endelevu ni kiungo kikubwa katika nchi kinachowasaidia wananchi kupiga hatua kutoka sehemu moja kwenda nyingine hivyo ni lazima serikali kuhakikisha kunakuwepo utawala bora wenye kufuata sheria ili kuweza kufikia malengo na mikakati ya kukua kwa uchumi nchini.

Nao watoa mada katika kongamano hilo walisema lengo la kukutana kwao ni kubadilishana uzoefu katika masuala ya kiuchumi jambo ambalo litaweza kuisaidia serikali katika kupambana na umasikini na kukuwa kwa uchimi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akiwasilisha mada kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu, Dk. Auric Kubuli, alisema Sekta ya Uchumi wa Buluu ni muhimu kwa uchumi na maendeleo endelevu visiwani Zanzibar kwa kuzingatia ushirikishwaji, mazingira rafiki, rasilimali watu na vifaa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi

# Marekani yamfagilia Dk. Samia

## ■ Yaahidi makubwa sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi (PEPFAR), umeipongeza Serikali yaAwamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuimarisha huduma za afya nchini.

Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Marekani imeahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuboresha zaidi huduma za afya.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Msaidizi ambaye pia ni Kaimu Naibu Mratibu Mkuu wa masuala ya Ukimwi wa Mfuko huo, Dk. Rebecca Bunnell.

Bunnel aliongoza ujumbe maalumu uliotembelea Mkoa wa Tanga katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa, Waziri Kindamba na Kituo cha Warahibu wa Dawa za Kulevya kilichopo jijini Tanga.

Aidha, pongezi hizo zimekuja wakati kasi ya maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) nchini, imepungua kutoka asilimia saba mwaka 2003 hadi kufikia asilimia 4.3 mwaka jana.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, akimwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliuongoza ujumbe wa wageni hao kutoka Marekani.

"Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha huduma za afya, hasa katika huduma jumuishi kwa waathirika wa dawa za kulevya na VVU," alisema Dk. Magembe.

Aidha, Dk. Magembe alisema kupitia ufadhili wa PEPFAR, Tanzania imeanzisha vituo tisa vya utoaji wa dawa ya Methadone kwa waathirika wa dawa za kulevya nchi nzima pamoja na huduma ya kliniki ya kutembea katika vituo saba.

"Tunaishukuru Serikali ya Marekani kwa msaada wake kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi kwa kuendelea kushirikiana katika uboreshaji wa huduma za afya nchini na mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi," alisema Dk. Magembe.

Kwa upande wake, Dk. Rebecca aliishukuru Serikali ya Tanzania kumkaribisha kuja kuona shughuli za PEPFAR mkoani Tanga na pia alishukuru kwa ushirikiano unaonyeshwa na Serikali ya Tanzania katika mapambano ya VVU na Ukimwi nchini.



# ... Wafanyabiashara wampongeza kufungua milango ya majadiliano



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Taifa (JWT), Hamis Livembe, akizungumza na wafanyabiashara (hawapo pichani), kuhusu kufanya kazi kwa bidii baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuifungua nchi kiuchumi.
Picha: Mpigapicha Wetu.

**Na Mwandishi Wetu, Kisarawe**

JUMUIYA ya Wafanyabiashara Taifa (JWT), imewataka wafanyabiashara nchini kufanya kazi kwa bidii kwa sababu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amefungua milango ya majadiliano na ameifungua nchi kiuchumi. Mwenyekiti wa JWT, Hamis Livembe, aliyasema hayo wakati akizungumza na wafanyabiashara wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani, katika mwendelezo wa ziara za viongozi wa jumuiya hiyo kusikiliza kero za wafanyabiashara nchi nzima.

Alisema wana wajibu wa kujivunia juhudi za Rais Samia katika kushughulikia kero zao na kufungua milango ya majadiliano, jambo ambalo halikuwahi kufanyika miaka ya nyuma.

Alisema awali wafanyabishara walikuwa hawana nafasi ya kusikilizwa isipokuwa inapotokea migomo na maandamano, lakini tangu utawala wa Rais Samia, wamepewa nafasi ya kujisemea na kusikilizwa.

"Tutembee kifua mbele, tufanye biashara kwa amani na utulivu, bila kusahau kutimiza wajibu wetu. Tumekutana hapa leo (jana) tujadili matatizo yetu, kipi kinatukwamisha kufanya biashara kwa utulivu ili kwa kushirikiana na serikali, tukae meza moja na tuyamalize," alisema.

Akitoa mfano wa moja ya kero ambazo imefanyiwa kazi ni faini ya kutokutoa risiti kwa mteja au kutoandika jina ambayo awali ilikuwa Sh. milioni 4.5, lakini imeshushwa hadi Sh. milioni 1.5 baada ya wafanyabishara kulalamika.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Uongozi ya JWT, Ismail Masoud, alisema katika mikoa 12 waliyopita, wamesikiliza kero nyingi ambazo zinafanana na tayari nyingine zimeanza kufanyiwa kazi.

Nao wafanyabiashara wa Wilaya ya Kisarawe, walilalamikia kodi za kero zinazotozwa na halmashauri na TRA ikiwamo ya jengo la fremu anayotozwa mpangaji badala ya mwenye nyumba.

Ziara hiyo inaendelea katika wilaya za Kibiti na Mkuranga mkoani humo.

# Rais IPU ajipanga kutoa tamko vita Mashariki ya Kati



**Na Hellen Mwango**

RAIS wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, amesema anajipanga kutoa tamko kuhusu vita vinavyoendelea Mashariki ya Kati kati ya Israel na wanamgambo wa Hamas wa Palestina.

Dk. Tulia ambaye ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyasema hayo wakati akizungumza na kituo kimoja cha redio jana asubuhi.

Akizungumzia baadhi ya majukumu yake, Dk. Tulia alisema, "Pamoja na mambo mengine, tunashughulikia mambo mengi ikiwamo kuhamasisha amani.

"Sasa hivi kuna vita nchi za Mashariki ya Kati ni jambo ambalo watu wanasubiri Rais wa IPU nitasema nini, ninajipanga, mtasikia nini nitasema, si jambo dogo, likitoka tamko ni Rais anasema kutoka Tanzania."

Akizungumzia ubadhirifu wa fedha za umma; Dk. Tulia ambaye ni Spika wa Bunge la Tanzania, alisema bunge linafanya mabadiliko ya namna ya kuhakikisha wananchi wanapata taarifa ikiwamo kujua kwamba bunge linaisimamia serikali katika matumizi ya fedha za umma.

Alisema yanapotokea matumizi mabaya ya fedha hizo ama ubadhirifu lazima hatua zichukuliwe.

Akifafanua zaidi alisema bunge linapopitisha maazimio linaiagiza serikali isipokuwa wananchi hawapati mrejesho kuhusu hatua zilizochukuliwa, lakini naamini tutafika huko katika maboresho.

Akizungumzia mazimio ya 2022 yaliyofanyiwa kazi na kukamilika alisema ni asilimia 47 kati ya 100, na kwamba si mbaya, tayari wanaweza kujua mangapi yameshafanyiwa kazi, haya mengine 53 Bunge tunapata fursa ya kufuatilia na yatanafanyiwa kazi.

"Yapo maagizo ya muda mfupi na ya muda mrefu, yale yanayolalamikiwa, sheria ifanyiwe mchakato, hatuwezi kusema leo halafu yakafanyiwa kazi kesho, lazima mchakato ufanyike ili kukamilisha," alisema.

Alisema katika taarifa hiyo serikali ilishapeleka mahakamani kesi zaidi ya 1,500 hizo ni nyingi na tayari 165 zimeshasikilizwa na kutolewa hukumu.

## Mbunge ahoji ujenzi vituo vya afya kuweka uwiano



**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, ameihoji serikali ni lini itajenga vituo vya afya katika Kata ya Misughaa na Issuna ili kuweka uwiano mzuri wa wananchi kupata huduma za afya.

Mtaturu aliuliza swali hilo jana Bungeni jijini Dodoma, katika swali la msingi lililoelekezwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

"Ninataka kujua Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Singida Mashariki lina Kata 13, lakini kati ya hizo ni moja ndiyo ilijengwa kituo cha afya, je, ni lini serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Misughaa na Issuna ili kuweka uwiano mzuri katika mkakati wa afya," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Festo Dugange, alisema mpango wa serikali wa kujenga vituo vya afya ni mkakati endelevu.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea kutafuta fedha kupitia mapato ya ndani ya Serikali Kuu, kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri na wadau mbalimbali kuhakikisha yale maeneo yaliyoainishwa ya ujenzi wa vituo vya afya kimkakati vinajengwa vituo hivyo.

"Ninakuhakikishia Mheshimiwa Mtaturu kuwa nitatoa kipaumbele katika Kata alizoziainisha ili ziweze kupata vituo vya afya," alisema.

## Bashungwa aagiza ukarabati mifereji

**Nitumie nafasi hii niwaelekeze mameneja wa mikoa Tanroads kote nchini kwenda kwenye maeneo ambayo yana changamoto kama wabunge walivyosema na kuleta haraka iwezekanavyo namna ambavyo tunaweza tukakabiliana na jambo hili kwa dharura.**

**Na Godfrey Sanga**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ametoa maelekezo kwa mameneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kukarabati mifereji iliyo pembezoni mwa barabara kuu ili kuzuia athari zinazoweza kujitokeza wakati wa mvua ikiwemo kuharibika kwa barabara.

Alisema hayo jana bungeni jijini Dodoma na kunukuliwa kupitia televisheni moja wakati akijibu swali la Mbunge wa Urambo, Margaret Sitta, aliyeuliza ni lini Wizara, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi itasafisha mifereji iliyozibwa wakati wa ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo.

"Nitumie nafasi hii niwaelekeze mameneja wa mikoa Tanroads kote nchini kwenda kwenye maeneo ambayo yana changamoto kama wabunge walivyosema na kuleta haraka iwezekanavyo namna ambavyo tunaweza tukakabiliana na jambo hili kwa dharura," alisema.

Naye Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima aliuliza ni lini ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka inayoanzia Mwenge kwenda Tegeta hadi Basihaya itaanza kujengwa.

Katika hatua nyingine, akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema hatua iliyopo kwa sasa ni hatua ya awali kwa ajili ya kuanza kujenga barabara na mkandarasi yupo eneo la ujenzi.

"Nimhakikishie mheshimiwa mbunge hatua iliyopo sasa hivi ni hatua za awali kwa ajili ya kuanza kujenga hiyo barabara na wakandarasi wapo wanafanya maandalizi ya awali kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo," alisema.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Tuzingatia sheria za barabarani



Tabia ya baadhi ya madereva kutofuata alama za barabarani zikiwemo pundamilia, tena kwenye maeneo nyeti yakiwemo ya wanafunzi wa shule za msingi ni ya kukemewa.

Wakati wengine tunaishia kukemea,vyombo vya dola vinapaswa kuchukua hatua.

Ushauri wangu kwa waendesha vyombo vya moto wote, ni muhimu kuzingatia alama za barabani pamoja na kuzingatia maeneo ya huduma za kijamii ili kuhakikisha hakuna ajali ya kizembe inatokea. Ni vizuri madereva wasiwe wanafuata sheria wanapomwona askari pekee bali kuzingatia sheria kila wakati.




## MAONI YA MHARIRI

# Tusibweteke, Ukimwi bado upo

NI habari njema kusikia kwamba kasi ya maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) nchini, imepungua kutoka asilimia saba mwaka 2003 hadi kufikia asilimia 4.3 mwaka jana.

Kwa lugha rahisi ni kwamba, katika kila watu 100, bado kuna watu takribani watano walio katika hatari ya kuambukizwa virusi vinavyosababisha ugonjwa huo ambao mpaka sasa hauna dawa ya uhakika.

Taarifa ya kushuka kwa maambukizi ya VVU Nchini, ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe.

Dk. Magembe anamwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuongoza ujumbe wa wageni kutoka Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi (PEPFAR) kwenda jijini Tanga kuangalia miradi inayofadhiliwa na mfuko huo.

Alisema nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kuimarisha huduma za afya, hasa katika huduma jumuishi kwa waathirika wa dawa za kulevya na VVU.

Pamoja na kasi ya maambukizi kushuka nchini, ni muhimu juhudi za kuhakikisha maambukizi ya ugonjwa huo yanashuka hadi sifuri zinaendelezwa. Yapo mengi yanayopaswa kufanywa na kila mmoja wetu, wadau, serikali za mitaa hadi Serikali Kuu ili kufikia hatua hiyo.

Baadhi ya hayo ni kuendelea kuwahamasisha wananchi kupima afya zao kwa hiari na kisha kuendelea kujilinda dhidi ya yale yanayoweza kusababisha mtu kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Elimu dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi, inapaswa kuendelea kutolewa kwani wananchi, hasa waishio maeneo ya vijijini, hawana elimu ya kutosha juu ya ugonjwa huo na athari zake katika jamii. Kwa kuwa sababu kubwa ya maambukizi ya VVU ni ngono zembe inayochangiwa na ulevi wa pombe na dawa za kulevya, serikali na wadau wanapaswa kuendelea kumulika maeneo ya aina hiyo na kutoa elimu.

Elimu pia inapaswa kutolewa kwa wananchi ili wasiwanyanyapae watu wanaoishi na VVU kwa kuwa tabia hiyo, licha ya kuwasababishia madhara ya kisaikolojia, inachangia wengi waendelee kujificha.

Juhudi za kuokoa watoto wanaozaliwa na wazazi wenye maambukizi ya VVU ili watoke salama zinapaswa pia kuendelezwa. Kwa hakika, kila mmoja akichukua jukumu lake ipasavyo, Tanzania bila Ukimwi inawezekana.

## Wasiliana nasi



| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255787559090 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |





Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
Sangagodfrey26@gmail.com

# Tuwe makini tunapoelekea kwenye chaguzi zijazo

TANZANIA iliamua kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992 ingawa kura ya maoni ilionesha kwamba waliotaka mfumo huo walikuwa asilimia 20 pekee ya Watanzania.

Hii ina maana kwamba kabla ya hapo mfumo huo ulikuwepo lakini ukafutwa na hivyo kwa takribani miaka 32, Tanzania ilikua ikiendesha mfmo wa chama kimoja.

Wakati Tanganyika inajipatia uhuru wake mwaka 1961 kulikuwa na vyama vingi vya siasa vya Tanganyika African National Union (TANU) kilichoanzishwa Julai 1954, United Tanganyika Party (UTP) kilichoanzishwa Februari 1956, All Muslim National Union of Tanganyika (AMNUT) kilichoanzishwa Julai 1959 na African National Congress (ANC) kilichoanzishwa Juni 1958.

Vyama hivi vilishiriki katika chaguzi za Baraza la Kutunga Sheria (Legco) mwaka 1958, 1959 na 1960. Hata hivyo, ni vyama viwili tu TANU na ANC vilivyoshiriki katika uchaguzi mkuu wa kumpata Rais wa Tanganyika uliofanyika Novemba 1, 1962.

Baada ya uhuru mwaka 1961, ndipo Tanzania ikaanzisha utaratibu unaoendelea hadi sasa wa madiwani, wabunge na Rais kuchaguliwa kila baada ya miaka mitano.

Madhumuni ya kurejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa yalikuwa yanalenga kuleta ushindani zaidi wa kisiasa, na hivyo kuleta maendeleo nchini. Kwa wanaokombuka hili ni jambo lilorejeshwa katika kipindi ambacho dunia ilikuwa inahimiza sana demokrasia ya vyama vingi na nchi nyingi zilikuwa zimeachana na mfumo wa chama kimoja.

Kimsingi, upinzani au ushindani wa kisiasa na sio uadui bali ni kuongeza wigo wa kushindinanisha sera ili yule mwenye sera nzuri apewe nafasi ya kuongoza nchi.

Baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, nchi yetu imeendelea kupita kwa amani katika chaguzi mbalimbali za kila baada ya miaka mitano, kuanzia mwaka 1995 bila uvunjifu wa amani.

Hii ni tofauti na baadhi ya nchi ambazo zimejikuta kwenye machafuko nyakati za uchaguzi wakiwemo baadhi ya majirani zetu.

Wakati tukielekea kwenye uchaguzi wa serikali za mtaa mwaka kesho na baadaye uchaguzi mkuu mwaka 2025 ni vyema kuanzia sasa tuanze kukumbushana kufanya siasa za kistaarabu ambazo zitajikita katika kutangaza sera lakini zikimwacha salama mama yetu Tanzania.

Ni vyema pia kuanza kuwakumbusha wapiga kura kukaa mkao wa kupata viongozi wapya ambao ni waadilifu na wenye nia thabiti ya kutumikia Watanzania na si kutumikia matumbo yao.

> **Baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, nchi yetu imeendelea kupita kwa amani katika chaguzi mbalimbali za kila baada ya miaka mitano, kuanzia mwaka 1995 bila uvunjifu wa amani.**

Ni vyema tuishi na kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kwamba "Uongozi na mzigo, mtu safi kabisakabisa hawezi kuukimbilia."

# Mwanamume, mwanamke wakutwa watupu wamefariki

**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

WAKAZI wawili wa Mtaa wa Imalanongwa A, Kata ya Mkwawa mkoani Iringa, Swiga John Mwakalobo (35) na Jacob Chang'a, wamekutwa wamefariki dunia ndani ya mgahawa wakiwa watupu.

Habari zilizopatikana eneo la tukio jana, zilidai marehemu Swiga alikuwa akifanya biashara katika mgahawa mmoja na kwa kawaida huwa anachelewa kufunga kutokana na maandalizi ya chakula cha asubuhi.

Wakielezea tukio hilo, baadhi ya majirani ambao hawakutaka majina yao kutajwa kwenye gazeti, walidai kuwa hadi ilipofika asubuhi, hawakuwa wamemuona Swiga.

"Tulifanya juhudi za kumtafuta kwa kumpigia simu mume wake bila mafanikio, simu yake ilikuwa ikiita tu bila kupokelewa, ndipo tulipoamua kwenda mgahawani kwake na tulipopiga tena simu tulisikia inaita ikiwa ndani huku mlango ukiwa umefungwa.

"Tulichungulia kupitia sehemu yenye uwazi, tukaoona miili miwili ipo ndani ambayo ilikuwa mitupu, tukavunja mlango," alisema jirani mmoja.

"Ndani ya mgahawa, tulikuta jiko la mkaa na maharage ambayo yalikuwa yamebandikwa sasa labda kilichowaua ni moshi wa mkaa (sumu ya hewa ukaa) uliowazidia wakiwa wamepitiwa na usingizi au wakiwa katikati ya tendo, wengine wanahisi labda walikuwa," Mwenyekiti wa Mtaa wa Imalanongwa A, Hamis Chananja, alithibitisha kutokea kwa kwa tukio hilo katika eneo lake na alisema polisi walifika kuchukua miili hiyo kwa uchunguzi zaidi.



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu kutoka mkoani Kagera, Neema Lugangira Bungeni jijini Dodoma jana. Picha: (Mpigapicha Wetu)

# MSD yakabidhi vifaa tiba vya mil. 900/-

**Na Mwandishi Wetu**

BOHARI ya Dawa (MSD), imekabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 900 kwa Halmashauri ya Ifakara Mji.

Mbunge wa Kilombero, Abubakar Asenga, alisema ujio wa vifaa hivyo, utasaidia kuboresha huduma za afya hivyo wanaishukuru serikali kwa hatua kubwa ya maboresho katika sekta hiyo.

Alieleza kuwa, jimbo hilo lilikuwa na kero saba kubwa ambazo hazijawahi kutatuliwa tangu kupata Uhuru lakini Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amezitatua ikiwemo mradi wa ujenzi wa barabara, maji, ukarabati kituo cha umeme Kidatu, ujenzi wa shule za kata, vituo vya afya, zahanati na hospitali.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyobya, alisema ujio wa vifaa tiba hivyo ni neema kwa halmashauri hiyo.

Alisema, maboresho hayo makubwa yanayofanywa na Rais Dk. Samia ni lazima kuungwa mkono na watendaji hivyo anatoa siku 15 kuhakikisha MSD inafunga vifaa hivyo na wananchi wanaanza kupata huduma.

"Niwaombe MSD ilete wataalamu wao kwa ajili ya kufunga vifaa hivi, haiwezekani Rais wetu afanye mambo makubwa kama haya watendaji tumuangushe, ni muhimu kuhakikisha tunasimamia na wananchi wanaanza kupata huduma kwa wakati," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa MSD ambaye ni Mfamasia na Afisa Huduma kwa Wateja Kanda ya Dar es Salaam, Diana Kimario, alisema kanda hiyo ina hudumia mikoa mitatu ambayo ni Pwani, Morogoro na Zanzibar ambapo Ifakara ni mnufaika.

"Ujio wa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 900 ni muendelezo wa mabadiliko makubwa katika maboresho sekta ya afya, sisi watumishi ndani ya MSD tunajivunia namna serikali yetu chini ya Rais Dk. Samia na Mkurugenzi wa bohari Mavere Tukai wanavyohakikisha tunafanya kazi bila hofu.




# Wataalamu Mahakama wapata uzoefu Tehama Kazakhastan

**Na Tiganya Vincent, Kazakhstan**

WATAALAMU wa Mahakama ya Tanzania wametembelea Kazakhastan, kubadilisha uzoefu kuhusu uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ili kuboresha shughuli za kila siku za utoaji wa haki nchini.

Timu hiyo inayoongozwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel, imetembelea Mahakama ya Juu ya Upeo (Supreme Court) ya Kazakhastan ambapo ilipata fursa ya kutembelea chumba maalum cha kusimamia, kuendesha na kudhibiti mtandao na kituo cha kuchakata taarifa za kimahakama kwa ajili ya kujifunza.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Prof. Ole Gabriel alimweleza Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Kazakhstan, Nail Akhetzakirov kuwa tukio hilo ni mwendelezo wa iliyofanyika mwaka 2018 ambapo watajifunza uendeshaji, usimamizi wa shughuli za Mahakama kwa kutumia Tehama

Alisema Kazakhastan imepiga hatua katika matumizi ya Tehama katika shughuli mbalimbali za Mahakama, hivyo nao watabadilishana uzoefu ili kuendeleza mapinduzi makubwa yanayoendelea ya Mahakama Mtandao nchini ikiwemo kupunguza matumizi ya karatasi katika uendeshaji wa shughuli zake.

Aidha, Prof. Ole Gabriel alimuomba Mtendaji Mkuu mwenzake wa Mahakama ya Kazakhastan kuendelea kushirikiana kwa maafisa Tehama wa pande zote kwa kubalishana uzoefu kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili waweze kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia hiyo yanayobadilika kila wakati duniani.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Kazakhastan aliishukuru timu ya Tanzania kwa ziara hiyo ya kubadilisha uzoefu na kuahidi kuendelea na ushirikiano utakaowezesha pande zote mbili kuimarisha zaidi matumizi ya Tehama mahakamani.

Awali, Prof. Ole Elisante na timu yake walipata fursa ya kutembelea Ofisi za Benki ya Dunia na kukutana na Mwakilishi wa Kazakhstan Andrei Mikhnev.

Viongozi wengine waliopo katika ziara hiyo ya mafunzo ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Jenifa Omolo, Jaji wa Mahakama Kuu, Angelo Rumisha na Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Alesia Mbuya.

# Ugomvi, dharau zavunja ndoa ya wakazi Mbeya

**Na Zawadi Kapambwe, Mbeya**

MAHAKAMA ya Mwanzo Mjini Mbeya, imevunja ndoa baina ya Gideon Siame Charles (32) na Wiven Simkonda (30), wakazi wa jijini Mbeya.

Akitoa hukumu hiyo Hakimu Miriam Kamwaga wa mahakama hiyo, alisema baada ya kusikiliza kwa kina pande zote mbili, aligundua kuwa ndoa hiyo kamwe haiwezi kurekebishika tena baina ya wadaiwa.

"Ndoa inaunganishwa na watu wawili yaani mke na mume, kadhalika ndoa hiyo hiyo inavunjwa na watu hao hao, yaani mke na mume," alisema.

Awali, ilidaiwa kuwa mdai Gideon alifika makakamani hapo kudai talaka kwa madai kuwa wamekuwa na ugomvi wa mara kwa mara na usio rekebishika.

Alisema mbali na kutoelewana, mdaiwa amekuwa akimdharau kupita kiasi, kitendo ambacho kinamfanya akose kujiamini kama mwanaume.

Hakimu Kamwaga alivunja ndoa hiyo na kuwaambia kwamba kila mtu yupo huru kuoa ama kuolewa.

> **Ndoa inaunganishwa na watu wawili yaani mke na mume, kadhalika ndoa hiyo hiyo inavunjwa na watu hao hao, yaani mke na mume,"**

# Hifadhi ya Taifa Ruaha yatoa magodoro 41 kwa wafungwa



**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

HIFADHI ya Taifa ya Ruaha, imekabidhi magodoro 41 kwa ajili ya malazi kwa wafungwa katika Gereza Kuu la Iringa.

Akikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Gereza la Iringa, Daniel Mwakapila, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, Godwell Meing'ataki, alisema jana kuwa msaada huo ni mchango wa faida zinazotokana na utalii.

"Mara nyingi tumekuwa tukijihusisha zaidi na miradi ya maendeleo kwa wananchi wanaozunguka hifadhi zetu, hivyo leo (jana) tumeona tutoe magodoro ikiwa ni mchango wetu kwa wenzetu wanaotumikia makosa yao," alisema.

Aidha, alisema msaada huu ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya Hifadhi ya Taifa Ruaha na Gereza Kuu la Iringa na kwamba Tanapa inawathamini wafungwa walioko magerezani.Kwa upande wake, Mwakapila, alisema, "Tanapa ni wadau wazuri sana kwetu na tunashirikiana nao katika mambo mengi, pia tuwashukuru kwa msaada huu ambao utatuondolea adha iliyokuwepo licha ya kwamba hautamaliza tatizo lote ila utasaidia kwa kiasi kikubwa."

Magodoro hayo 41 yamekabidhiwa leo tarehe 06.11.2023 katika Gereza Kuu la Iringa.

# Jaji: Dhihirisheni umma haki ni ukweli unaopatikana

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imewataka wajumbe wa Baraza la Maadili kusimamia haki na kuudhihirishia umma kuwa haki siyo dhana, bali ni ukweli unaopatikana kwa kila mhusika.


Hayo yalisemwa na Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, ambaye ni Kamishna wa Maadili, Sivangilwa Mwangesi jijini Arusha jana, katika hotuba yake ya ufunguzi wa mafunzo ya siku tano kwa wajumbe wa Baraza la Maadili iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri Kipacha ambaye ni Katibu Ukuzaji wa Maadili, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Kama wajumbe wa Baraza la Maadili ninyi ni kiunganishi kati ya sheria na watu wanaolengwa kusaidiwa na sheria. Mnatakiwa kuuhakikishia umma kwamba haki siyo dhana bali ni ukweli unaopatikana kwa kila muhusika," alisema.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Maadili, jukumu la wajumbe wa Baraza la Maadili ni muhimu katika eneo la uadilifu wa vingozi wa umma kwa sababu wao ndio husimamia haki, kuhakikisha usawa na kuimarisha utawala bora ndani ya jamii yetu.

"Jukumu lenu linachukuliwa kwa uzito mkubwa ndio sababu tuko hapa. Mnabeba jukumu kubwa linalogusa maisha ya wananchi kwa mahusiano yao na Serikali yao. Mnayofanya yanatoa mwelekeo wa haki na kazi yenu inaathiri maisha ya watu wanaokuja mbele ya Sekretarieti ya Maadili kutafuta haki na ufumbuzi wa malalamiko yao kuhusiana na Viongozi wa Umma," alisema.

> **Jukumu lenu linachukuliwa kwa uzito mkubwa ndio sababu tuko hapa. Mnabeba jukumu kubwa linalogusa maisha ya wananchi kwa mahusiano...**



Aidha, wajumbe hao wa Baraza la Maadili, katika kipindi hiki cha mafunzo yanayohusu utekelezaji wa majukumu yao, watapitishwa katika mada mbalimbali ikiwa ni pamoja na utambuzi wa makosa ya kimaadili, namna ya kushughulikia mashauri yanayowasiishwa mbele ya Baraza na kupata uzoefu kutoka mataifa mengine duniani.

Mafunzo hayo yanafanyika chini ya ufadhili wa programu endelevu ya kujenga uwezo kwa taasisi katika kupambana na rushwa nchini (BSAAT).

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

# JARIDA Jungu Kuu

| Jumatano Novemba 8 - 14, 2023 |







# Zitto Kabwe alivyo sahihi kutosusia chaguzi

UK. 12 & 13

# Kuna tija gani kuchafuana kwa jambo linaloibeba nchi yetu?

**Na Reubeni Lumbagala, Kongwa**

UJENZI wa nchi si kazi ndogo wala lelemala. Kuijenga nchi ni kazi ngumu inayogharimu raslimali fedha, watu, muda na mawazo bunifu.

Kwa kifupi, kujenga ni kazi ngumu kuliko kubomoa. Tangu nchi yetu ipate uhuru wake Desemba 9, 1961, juhudi kubwa inayofanyika ni ujenzi wa nchi kijamii, kiuchumi, na kisiasa.

Kwa vile Tanzania si kisiwa, ujenzi wa nchi pia unahusisha kujenga mahusiano mazuri ya nchi yetu na nchi nyingine.

Ni katika muktadha huo, Tanzania imekuwa mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa kwani yapo manufaa mengi kujenga mahusiano mazuri baina ya nchi yetu na jumuiya ya kimataifa.

Ujenzi wa nchi na kuifanya uhusiane vyema na jumuiya ya kimataifa si kazi ya viongozi peke yao bali ni kazi ya kila raia, yaani viongozi wetu pamoja na wananchi wote.

Kama wahenga wasemavyo "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu" ndivyo ushirikiano wa pamoja wa viongozi na wananchi ulivyo nguzo muhimu ya kufanikisha ujenzi wa nchi yetu kwa maendeleo endelevu ya kizazi cha sasa na kijacho.

Tukiwa na sauti moja na tukiwa na nia moja, ni dhahiri kama nchi tutafanikiwa kwa haraka sana katika jitihada za kujiletea maendeleo.

Kwa mtazamo wangu, hapo nyuma, hususan kipindi baa la Uviko - 19 linasumbua dunia, uhusiano wetu na baadhi ya mataifa ya nje, ulilegalega kidogo, pengine kutokana na misimamo yetu huku wengine wakishindwa kutuelewa.

Lakini Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Dk. Samia Suluhu Hassan imekuwa na vipaumbele vingi katika kufanikisha maendeleo ya nchi na uhusiano wetu na mataifa mengine.

Moja ya kipaumbele cha Rais Samia ni kuifungua nchi kimataifa na hivyo kuhimiza diplomasia ya uchumi.

Mwanadiplomasia huyu namba moja nchini, amekuwa akihimiza nchi yetu kujenga mahusiano mazuri na mataifa mengine kwa ajili ya manufaa ya pamoja.

Mabalozi wetu wanaotuwakilisha katika nchi mbalimbali ulimwenguni wamekuwa wakihimizwa kufanya kazi kwa bidii hasa katika kutafuta fursa ambazo zitainufaisha nchi yetu ili kuchagiza gurudumu la maendeleo. Pia wanahimizwa kuvutia wawekezaji kuja Tanzania kwa wingi ili kuwekeza na hivyo kutengeneza ajira.

Kimsingi, juhudi kubwa zinafanyika kuifungua nchi yetu kimataifa kwani kufanikiwa kwa hili, kuna uhusiano wa moja kwa moja na kufanikisha mipango ya kimaendeleo kwa ustawi wa nchi na raia wake.

Ushiriki wa Tanzania katika uchaguzi wa kumtafuta Rais wa Umoja wa Mabunge Dunaini (IPU) ulikuwa ni fursa nyingine kwa nchi yetu kujitangaza kimataifa.

Katika uchaguzi huo ambao umezidi kuitambulisha Tanzania kimataifa, Spika wa Bunge letu, Dk. Tulia Ackson ndiye aliyepeperusha bendera ya nchi yetu, na Mwenyezi Mungu akawa upande wake na kushinda kwa kishindo uchaguzi huo.

Hata hivyo, kumbe mambo hayakuwa rahisi, na ugumu wa kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia kwa Dk. Tulia ukawa unawekwa na Watanzania wenyewe!

Ni vigumu kuamini kwamba wapo Watanzania walioamua kumchafua Spika wetu ili asichaguliwe kushika nafasi hiyo ambayo kwetu ni turufu muhimu kufanikisha azma ya serikali kuifungua nchi kimataifa.

Ukweli huo uliwekwa hadharani Oktoba 30, 2023, katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma kwenye hafla ya kumpongeza Dk. Tulia kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na pia kuingia kwenye rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Tulia Ackson alieleza namna alivyokutana na magumu wakati wa uchaguzi huo huku baadhi ya Watanzania wakiwa kinyume nae.

"Uchaguzi ule ulikuwa mgumu sana na hii ni kutokana na mitandao ya kijamii kutumika kunichafua. Tena waliofanya hivyo ni Watanzania wenzetu ambao walikuwa wakiungana na watu wengine ili tu nisishinde kwenye nafasi hii," anasema Dk. Tulia.

Kiukweli inashangaza sana kuona fursa adhimu tuliyoipata tunataka kuipiga teke kwa kumchafua mgombea wetu ambaye ushindi wake unatangaza nchi yetu katika uga wa diplomasia.

Ushindi wake pia ni darasa muhimu katika kuhamasisha wasichana na wanawake kujiamini katika nyanja zote mbali na kuzidi kuitangaza nchi kimataifa.

Kasumba hii mbaya ya kuchafuana si jambo jema hasa linapokuja suala la kitaifa lenye maslahi kwa nchi yetu. Mtu unajiuliza, hivi kumchafua Mtanzania mwenzako katika kinyang'anyiro kama hicho inakuwa inatokana na wivu, husuda, uadui au ujinga? Nimejiuliza sana.

Kuungana na adui dhidi ya ndugu yako ni kukosa uzalendo. Ni katika muktadha huo, Dk. Tulia aliendelea kusema: "Ni jambo la ajabu sana Watanzania kuungana na adui zetu kulipiga vita taifa letu. Niwaombe linapotokea suala la kitaifa tuwe kitu kimoja badala ya kuungana na adui zetu kuumizana wenyewe kwa wenyewe."




Anasema nchi nyingi zilisema hazitaingiza wagombea ili kuipa nafasi Tanzania kuchukua kiti cha urais cha umoja wa mabunge lakini maneno ya kwenye mitandao yakawapa nguvu ya kuleta wagombea! "Lakini kwa kuwa Mungu alikuwa amepanga Tanzania ishinde hakuna kilichobadili hilo," anasema.

Kasumba hii ya ajabu nimeiona pia katika sekta ya michezo. Inapokuja timu kutoka nje ya nchi kucheza na timu zetu, hususani zile zinazofahamika kama kubwa, baadhi ya mashabiki wa Tanzania hushabikia timu ya nje na kuacha kushabikia timu ya ndani. Wanafanya hivyo huku wakijua au kutojua kwamba matokeo yoyote mazuri ni faida kwa nchi mbali na klabu husika.

Kwa mfano, matokeo mazuri ya timu zetu katika mechi za kimataifa yamesababisha timu zetu nyingi kushiriki mashindano ya CAF na hata baadhi ya timu zimetolewa lakini jina la Tanzania limetajwa na timu zimepata uzoefu.

Ushindi wa timu zetu katika mechi za kimataifa, unaongeza kujiamini (confidence) na hata kuwafanya wapinzani watuogope pia tofauti na zamani walipokuwa wanatudharau sana na wanapocheza na sisi huwa na asilimia 100 ya confidence.

Bila shaka, kushabikia timu zetu hizi kubwa si uadui na hivyo tunaweza kuombeana mabaya na kukinzana tunapocheza ligi ya ndani lakini zinapokutana na timu za nje, ni vyema tuoneshe uzalendo. Kama uzalendo ukikushinda, kaa kimya na si kumshangilia au kumrahisishia mgeni amshinde mwenyeji.

Tanzania ndiyo nyumba yetu, ni vyema viongozi na wananchi kwa pamoja tuijenge nyumba yetu-Mama Tanzania, ipendeze kwenye macho ya wageni hata kama kwa ndani tuna misuguano yetu.

Linapokuja suala la kuvutia nchi yao kwenye diplomasia ya uchumi baadhi ya majirani zetu hawana utani kwa sababu wanajua hilo lina faida kwao na vizazi vijavyo. Wapo waliofikia kusema uongo kwamba Mlima Kilimanjaro hauko Tanzania bali nchini mwao!

Wakasema tena uongo kwamba hata Olduvai Gorge ambako fuvu la mtu anayesadakika kuwa wa kale zaidi duniani lilivumbuliwa, haiko Tanzania bali kwenye nchi yao!

Juzijuzi mashindano mapya ya African Football League (AFL) yalipofunguliwa Tanzania na kuvuta dunia kuja au kuiangalia Tanzania, vichwa viliwauma sana hao majirani zetu kwa mujibu wa habari za mtandao.

Kufanikiwa kwa ujenzi wa nyumba yetu kutategemea sana umoja na upendo baina yetu. Hatupaswi kugombania fito wakati tunajenga nyumba moja. Kusimama kwa nyumba yetu ni sifa yetu sote na kubomoka kwa nyumba yetu na kuonekana chafu mbele ya macho ya wageni ni fedheha kwetu sote.

Likija jingine lenye sura ya utaifa, tusirudie makosa kama anayomlalamikia Dk. Tulia. Ni kwa kudra za Mwenyezi Mungu, hili limepita salama kwamba pamoja na kuchafuliwa kwake lakini Dk. Tulia ameshinda kwa kishindo.

Tuwe wazalendo kwa nchi yetu, tuwe wamoja, tuungane pamoja kwa mambo ya kitaifa, leo yetu ndiyo kesho yetu. Tafakari, chukua hatua.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni 0620 800 462.***

Kolamu



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Mkiendelea hivyo filamu zenu hazitakuwa na kishindo ng'o

**Na Hamisi Kibari**

HIVI karibuni, kulikuwa na uzinduzi wa tamthilia mpya ya Lawama, uzinduzi ambao ulienda sambamba na tangazo kwa wadau wa filamu kwamba kuanzia

Januari, mwakani, Azam itaanza kupokea filamu kutoka kwa watayarishaji nchini.

Mkuu wa Chaneli ya Sinema Zetu, Sophia Mgaza, alisema safari hii wanataka kuanza mwaka 2024 kwa kishindo kwa kupata filamu bora za Bongo.

Baadhi ya vigezo alivyotaja ni mtu kuja na wazo la kipekee la hadithi, kueleza wahusika tarajiwa na sifa zao, mandhari tarajiwa na mwonekano wa filamu.

Pia mtayarishaji kutoa maelezo mafupi kutoka kwa mzalishaji na mwongozaji wa filamu, kuainisha timu itakayohusika katika uzalishaji pamoja na mwongozo (script).

Vigezo vingine vitakavyoangaliwa alisema ni ushahidi wa kazi zilizowahi kufanywa na mzalishaji na mwongozaji, mpango wa uzalishaji wa filamu husika, bajeti inayotarajiwa kutumika katika uzalishaji wa filamu kwa kugusa kila hatua na kuwasilisha uthibitisho wa hadithi na mwongozo.

### HATUA YA KUPONGEZWA

Ninawapongeza Azam kuja na utaratibu huu. Wakiusimamia kwa uwazi na bila upendeleo wa kuangalia majina ya watu, matarajio yangu ni kupata filamu nzuri zenye viwango vya kimataifa katika nchi yetu.

Kwa sababu filamu ni biashara, ni ajira na maokoto kwa serikali, hatua hii ya Azam ni ya kuungwa mkono na kila mdau kwani inakwenda kuleta nmanufaa mengi kwa Watanzania.

Nilivyoelewa mimi filamu zitakazopatikana zitauzwa pia nje, hususan katika vituo vya televisheni na kuingiziwa lugha mbalimbali kama ambavyo sasa hivi inafanywa kwa kwenye filamu za Kiingereza, Kituruki, Kihindi, Kichina na kadhalika na kuziingizia Kiswahili.

Taarifa ya Shirika la Elimu na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) ya mwaka 2022 inaitaja Nigeria kama nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa filamu Afrika, ikizalisha takribani filamu 2,500 kwa mwaka ikifuatiwa na Ghana kisha Afrika Kusini. Tanzania ni ya saba ikizidiwa na Kenya ambayo ni ya sita.

Taarifa inasema tasnia ya filamu Afrika inaingiza Dola za Marekani bilioni 5, ikiajiri watu milioni 5, lakini ikisimama sawasawa inaweza kuingiza Dola za Marekani bilioni 20 na kuajiri watu milioni 20.

Hivyo serikali, wadau mbalimbali na vituo vingine vya televisheni nchini vinapaswa pia kuja na mpango kama huu.

Imani yangu ni kwamba hatua hii ya Azam itakwenda hadi kwenye michezo yakuigiza ili kupata michezo mizuri zaidi ya watayarishaji wa ndani inayokwenda sawia na maadili na utamaduni wetu.

Kwa mfano, si utamaduni wetu mtoto kumfokea mzazi hata kama mzazi amakosea. Hili kwa Wazungu ni kawaida na hata mchezo mmoja wa Kituruki niliouangalia hivi karibuni hili linajitokeza!

### KIANGALIENI UPYA KIPENGERE HIKI

Ushauri wangu kwa Azam ni kipengere cha mleta maombi kuonesha ushahidi wa kazi zilizowahi kufanywa na mzalishaji na mwongozaji kisije kikatumika kuwaengua watu ambao wanaweza kuzalisha filamu nzuri kwa kiwango cha kimataifa hata kama huko nyuma hawajawahi kuzalisha kutokana na sababu mbalimbali.

Kuna waliowahi kuzalisha filamu nzuri wakati teknolojia ikiwa VHS, kazi ambazo pengine hawana sasa hivi kama ushahidi, wakajikuta mawazo yao yametupwa kutokana na kigezo hicho. Mimi mmoja wao.

### WAZO LA HADITHI

Kwa watayarishaji filamu, kubwa la kuzungatia ni kupata hadithi nzuri. Hata siku anatangaza kuanza kupokea filamu, Sophia alisisitiza sana umuhimu wa hadithi nzuri.

Uchunguzi wangu kwa wenzetu walioendelea kwenye tasnia ya filamu wanasema pia kwamba ili filamu kufanya vizuri sokoni sifa kuu ni hadithi, pili ni mwongozaji wa filamu (director).

Kwamba hata watazamaji wanaposikia filamu imetoka, huwa wanaanza kuulizia mtunzi wa hadithi ni nani kama alishajidhihirisha kutunga visa vya kusisimua na kisha wanauliza mwongozaji.

Lakini huku kwetu watu wakisikia filamu mpya, wanauliza, kuna fulani, kuna Ray, kuna JB, kuna Bi Mwenda n.k.

### HADITHI ZA KUBABIA

Tatizo kubwa kwenye filamu zetu ni visa vilivyojengwa katika hadithi zisizovutia.

Uchunguzi wangu unaonesha watayarishaji wetu wengi ni waigizaji pia lakini hawana vipaji vya kutunga visa 'vikali' hivyo wanalazimisha kutunga na kwa kuwa wanajua soko letu 'jinga' linaangalia majina ya waigizaji kwanza! Hata wakipeleka kazi Azam, kitakachoangaliwa kwanza ni majina ya wahusika!

Kwa vile si watunzi, wanachokifanya wengi ni kuiba mawazo ya watu wengine na kubadili hapa na pale na kupata filamu.

Nalisema hili si kwamba ni hisia zangu tu bali nililishuhudia kwa macho yangu.

Niliwahi kumiliki chumba cha kuzalisha video na filamu kati ya mwaka 2005 hadi 2012 nikiwa na kijana mmoja akiitwa John Kalaghe ambaye sijui siku hizi yuko wapi na baadaye Hamisi Msekwa.

Kuna siku, mmoja wa wateja wetu ambaye siku hizi ni mzalishaji mkubwa wa filamu, alikuja na mikanda miwili ya filamu za ki-Nigeria, akamwambia Kallaghe 'Hebu angalia hizo filamu, tupate mchezo tufanye harakaharaka.'

Nilimshangaa, nikamuuliza kwa nini anafanya hivyo wakati anaweza kununua hadithi kwa Watanzania na nikamtajia baadhi ya watunzi ninaowajua. Akanijibu hawezi kupoteza hata Sh 10,000 kwa hilo!

Kwa hiyo utaona kwamba filamu zetu kwa muda mrefu, zimekuwa za kuiba mawazo ya wengine, kuiga au kubadilisha hadithi za filamu za nje.

Inadaiwa kwamba ili kupambana na vitendo vya uchawi na ushirikina vilivyokuwa vimekithiri Nigeria, baadhi ya makanisa yalifadhili filamu ambazo mwisho wa siku Yesu akawa anaushinda uchawi, lakini ajabu watengeneza filamu wa Bongo nao wakawa wanaiga kibubusa maudhui hayo.

Siku moja nilishangaa kuona filamu ya Bongo, ushirikina na uchawi ukiibuka 'kidedea'!

Katika matukio tofauti, mimi na mtunzi mmoja rafiki yangu, Chris Magori, tuliwahi kuona filamu ambazo wahusika walichukua mawazo yetu kutokana na hadithi tulizotoa kwenye magazeti, wakibadilisha kidogo sana.

Mwenzangu alifuatilia lakini akakwama huko mbele lakini mimi nilimwachia Mungu!

### HADITHI ZINAKOPATIKANA

Ndugu zangu watengeneza filamu, Tanzania haina ukame wa hadithi za kusisimua zinazoweza kuzalisha filamu nzuri.

Zipo hadithi za wakongwe kama Eddie Ganzel, Hammie Rajab, Ben Mtobwa, Faraji Katalambula, John Rutayisingwa, John Simbamwene na wengineo wengi ambazo mpaka sasa zikichezwa filamu zutateka soko.

Lakini pia kuna watunzi wa sasa ambao wana hadithi kali za kusisimua ambako watengeneza filamu wanaweza kwenda kununua.

Baadhi ya hao ni Hussein Tuwa, Maundu Mwingizi, Hussein Wamanywa, Lilian Mbaga, Fadhy Mtanga, Beka Mfaume, Patrick Massawe, Innocent Ndayanse, Laura Pettie, Chris Magori, Dickson Mtalaze, mimi mwenyewe na wengineo.

Ukiangalia katika vigezo ambavyo Azam wameweka, ni watayarishaji wa filamu kuonesha bajeti kuanzia ya uandishi wa hadithi. Kwa hiyo watayarishaji msisite kwenda kwa watunzi kununua hadithi nzuri.

Hata Marekani inayoongoza kwa kuzalisha filamu duniani, sehemu kubwa ya filamu zao zinatokana na vitabu na si watu kubadilishabadilisha mawazo ya wengine. Huo ni wizi (plagiarism) hata kama anayeibiwa kazi yake ni Mnigeria.

### FILAMU ZENYE MAADILI

Katika filamu mtakazotengeneza, Azam imehimizwa kuzingatia kufanya utafiti. Hili ni tatizo kubwa pia. Yaani watu wanashindwa kutafiti hata kitu kidogo sana kama vile kwenye Jeshi la Polisi nani anamwita mwenzake 'afande'. Niliwahi kuona filamu moja ya Bongo Mrakibu wa Polisi akimwita Koplo 'afande'.

Lakini kitu ambacho kwenye taarifa ya Sophia sikuona anahimiza ni maadili na utamaduni wetu kama Waafrika. Kuna baadhi ya filamu za Bongo huwezi kuzitazama mtu na familia yako. Zimejaa ukakasi. Usipohimiza hili siku moja unaweza hata kuletewa filamu zinazohamasisha ushoga.

Zingatieni pia uhalisia. Kwa mfano, toka nizaliwe sijawahi kuona Watanzania wakitoleana bastola kwa kupishana tu kauli. Tanzania ukisikia bastola mtaani basi ni tukio la ujambazi.

Niliwahi kuona filamu moja ya Bongo kila mtu kwenye baa ana bastola na si majambazi bali wahuni tu wa mjini. Ingekuwa wanatoleana visu nisingeshangaa.

Nikajiuliza hii ni Tanzania gani?

### SHIDA KWA WAONGOZAJI

Mwongazaji (director) ni sawa na kocha kwenye timu ya mpira wa miguu. Ana dhima ya kuhakikisha waigizaji wanavaa uhusika kwa mujibu wa mwongozo (script).

Lakini huku kwetu unakuta mwongazaji ndiye mwigizaji mkuu! Nasikia kuna waigizaji Tanzania wanasema "hakuna mtu wa kuniongoza' wakati kule India nasikia hadi leo Amitabh Bhachchan akiigiza anaongozwa na vijana wadogo!

Hili pia limesababisha waongozaji wa filamu ninaowafahamu kama Bishop Hiluka (pia ni mtunzi) na Chris Magori kukosa wa kuwaajiri!

Siasa



# Zitto alivyo sahihi kutosusia chaguzi

**Na Hamid Yassin**

KAULI ya Kiongozi Mkuu wa Chama cha Alliance For Change and Transparency (ACT - Wazalendo), Zitto Kabwe kuweka wazi kuwa, chama hicho kitashiriki uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwakani 2024 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 bila kujali kama Tanzania itakuwa imeandikwa katiba mpya au la ni ya kuungwa mkono.

Kiongozi huyo alitoa msimamo huo wakati akijibu mapigo ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu kwamba chama chao hakitashiriki uchaguzi wowote hadi kile wanachoita 'Katiba Mpya' itakapokuwa tayari.

Kiongozi huyo wa Chadema amekuwa akitoa kauli hiyo katika ziara zake za kukinadi chama hicho kupitia mikutano ya hadhara iliyoruhusiwa hivi sasa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Lissu pia amenukuliwa akidai kwamba, chama cha ACT-Wazalendo ni CCM B kwa madai kwamba hawapiganii ajenda ya Katiba Mpya kwa dhati, zaidi ya kuimba 'nyimbo' za kukisifu chama tawala, yaani CCM.

Mbali ya kutaka kauli hizo za Chadema kupitia Lissu kudharauliwa na kupuuzwa, Zitto amenukuliwa akiweka wazi kwamba, yeye binafsi na hata chama chao wamekuwa wakipagania katiba mpya hadharani na hakuna mtu anayeweza kuwachafua katika hilo.

"Nasikia Chadema wanasema kama katiba mpya haitakuwa tayari hadi kufikia mwakani basi watasusia chaguzi zote zijazo, nataka kuwaambia wananchi mapema kabisa kwamba sisi ACT Wazalendo kamwe hatutasusia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani wala ule Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 hata kama wataendelea kutuita CCM B," ametanabahisha Zitto Kabwe.

Akielezea sababu za kuchukua msimamo huo, kiongozi huyo ambaye ameshawahi kuwa mbunge kuanzia mwaka 2005 hadi 2015 kupitia Chadema, amedai umetokana na ombwe lililopo katika vikao vya maamuzi vya kitaifa kwa kukosekana wawakilishi kutoka vyama vya upinzani.

"Bunge letu la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi kule Zanzibar yamegeuka vyombo vya CCM kupitisha kirahisi ajenda zao, hii inatokana na idadi ndogo ya wabunge na wawakilishi wa kambi ya upinzani katika vyombo hivyo baada ya baadhi yetu kususia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Wacha waendelee kutuita CCM B, lakini sisi kamwe hatutasusia uchaguzi wowote ule kwa madai ya katiba mpya," alisisitiza Zitto Kambwe.

Aliongeza, "Kutokana na uzoefu wangu tangu kuanza kwa mfumo huu wa vyama vingi mwaka 1992, ni kweli vyama vya upinzani vimekuwa vikililia katiba mpya lakini si kwa utaratibu huu wa kususia chaguzi ulioasisiwa na Chadema."

Anachosema Zitto ni kweli kwamba chaguzi zilizopita ziliwaingiza bungeni wabunge wengi wa upinzani akiwemo Lissu mwenyewe kwa kutumia katiba iliopo.

Ni kweli pia anachosema Zitto kwamba vyombo hivyo vikubwa vya maamuzi vimekosa ule msisimko kama wakati vyama vya upinzani vilipokuwa na wabunge mahiri na machachari wa kupembua mambo na kujenga hoja wakati wa mijadala mbalimbali ndani ya Bunge na Baraza la Wawakilishi.

Kama vyama hivi vya upinzani vingekuwa vinasusia chaguzi zote tangu miaka ile, akina Lissu na wenzake, wangepata wapi fursa ya kuingia bungeni, hali ambayo mbali na kuwawezesha kutoa michango yao lakini pia iliwaongezea umaarufu wanaonufaika nao leo katika uga wa siasa.

Sasa ni miaka 31 na ushei tangu Julai Mosi mwaka 1992 wakati sheria namba 5 iliyounda vyama vingi vya siasa ilipoanza rasmi kufanya kazi, lakini bado wapinzani hapa nchini wanaendeleza siasa za maigizo ambazo zinaminya uhuru wa kifikra kwa wanasiasa wa vyama vyao.

Wanaendeleza siasa zinazolazimisha nyeupe ionekane buluu na nyekundu iitwe nyeusi na ukifanya kinyume chake lazima wenye chama chao wakuite majina ya kuudhi kama vile mnafiki, msaliti, umenunuliwa, mamluki

# Siasa

na kadhalika!

Kwamba chama cha upinzani hakitakiwi kuunga mkono lolote zuri linalofanywa na chama tawala na ukiunga mkono unaitwa CCM B si sawa

Pia si sahihi kwamba kile ambacho chama fulani cha upinzani kinaona ni sahihi kwao basi lazima vyama vyote vifuate na usipofuata basi wewe ni CCM B. Hili pia ni la kupuuzwa!

Kifo cha siasa kambi ya upinzani kinaweza kusababisha Tanzania kama nchi ikose wanasiasa makini wanaosaidia katika kujenga nchi makini. Ni kweli kabisa kwamba upinzani ukiwa makini, hukifanya pia chama tawala kisibweteke kwa kuongeza umakini.

Nchi yoyote inapokosa wanasiasa halisi yaani wanasiasa makini, lazima pia itakosa viongozi halisi kwa sababu siasa ya nchi ndiyo inazaa viongozi.

Wengi hawaujui uhusiano wa siasa ya nchi na uongozi wa nchi, hali yao ya kutojua haizuii mambo hayo mawili yasihusiane. Siasa ya nchi na uongozi wa nchi vinahusiana sawa na kuku na yai, kwamba kuku anataga yai nalo yai linalototoa kifaranga.

Kuku anapotaga yai nalo yai linamtoa kuku, mzunguko huo lazima uendelee, ukiharibiwa yaani akitokea mtu akausitisha upatikanaji wa mayai bora, lakini mtu huyohuyo akatamani kula nyama nzuri ya kuku yaani kuku walio bora, wajuao watamshangaa kwamba huyo anataka kula nyama ya kuku waliotoka wapi?

Kwa kuwa haiwezekani kuku waanguke kutoka juu mbinguni. Ni lazima yawepo mayai bora yanayototoa vifaranga walio bora. Hayo ndiyo yatamwezesha mlaji kupata maonjo ya nyama iliyo bora, hao kuku bora ndio wanaoweza kutaga mayai yaliyo bora na kuuendeleza mzunguko wa ubora.

Kususia chaguzi kwa vyama vya upinzani ni sababu moja kati ya kadhaa inazoharibu mzunguko wa kuku na yai! Utapata wapi viongozi bora wapya watakaopimwa na wananchi pasipo kupitia mfumo bora wa demokrasia wa kuchaguana?

Kimsingi, Watanzania wa leo huwezi kuwadanganya. Kama wewe umeonesha uadilifu wa hali ya juu na uwezo wa kuwawakilisha watakuchagua tu hata kama hakuna katiba kabisa alimradi kuna uchaguzi!

Kwa hiyo hakuna cha katiba mpya wala nini bali ni nini unawashawishi wananchi utakachowafanyia bungeni Chadema iliongoza vyama vya upinzani kususia uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, ulipofika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 wakatengeneza mizengwe ili baadhi ya wanachama wao wasusie kugombea ubunge, lakini kiongozi wao Tundu Lissu alichukua fomu za kuwania urais na alishiriki hatua zote!

Naungana na Kiongozi Mkuu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe kwamba zitafutwe mbinu nyingine za kuhimiza katiba mpya badala ya kususia chaguzi kwani ni kuwanyima fursa wananchi kuwa na machaguo mbadala.

Kuhimiza? Ndiyo, kwani Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia imeshapitisha rasmi azimio la kuandaa katiba mpya na kilichobaki ni utekelezaji na kimsingi chama tawala hakionekani kuwa na wasiwasi wowote kutokana na turufu yake ya kupeleka maendeleo kwa wananvhi.

Na ikumbukwe kwamba kuandika katiba si lelemama, ni mchakato makini unaohitaji muda wa kutosha na raslimali fedha!

Tundu Lissu na Chadema yake waendelee na 'blaablaa' zao! Wamesusia uchaguzi mdogo kule jimbo la Mtambwe Pemba, lakini wenzao ACT Wazalendo wametia timu uwanjani na kujinyakulia mwali mbele ya Chama tawala, CCM!

Ushauri wangu kwao, wangetumia kipindi hiki kutangaza sera zao mbadala zifahamike na kueleza kile ambacho wanaweza kuwapa Watanzania katika zama tulizinazo.

Sera za kusubiri watendaji wakuu wa serikali wateleze kama binadamu na wao wapandie hapo kupata kile vijana siku hizi wanaita kiki, hakitawasaidia lolote.

Pia sera za matusi na hasa kupinga kila kitu kinachofanywa na serikali iliyoko madarakani, sioni pia kama kitaisaidia chochote Chadema kufanya vizuri kwenye chaguzi zijazo hata kama katiba mpya itaandikwa leo.

Timu ya mpira wa miguu uwanjani, kwa mfano, inashinda kutokana na maandalizi mazuri na kuwa na wachezaji wazuri na si uwepo wa refa anayesimamia vizuri sheria. Hata refa akiwa mzuri vipi katika kusimamia sheria 17 za mpira, timu yenu ikiwa mbovu mtapigwa tu.

Kwangu mimi sheria za mpira ninazilinganisha na katiba ambayo bado zinaweza kuwepo nzuri ajabu lakini isiwasaidie lolote wapinzani kama hawana sera nzuri za kuonekana huku wao wenyewe wakionesha uongozi wa kutukuka na uadilifu.

Miaka kadhaa iliyopita majirani zetu wa Kenya waliibuka na katiba ambayo waliita huru, nzuri na wengine wakisema ni bora kuliko zote Afrika. Tuulizane leo, imesaidia vya kutosha wapinzani kuingia Ikulu? Lakini wapinzani Kenya waliwahi kuingia Ikulu kwa katiba ya zamani.

Kusema hivyo siyo kwamba ninapinga katiba yetu kuandikiwa upya, bali naonesha kwamba cha muhimu zaidi ni kuonesha wananchi unachotaka kuwafanyia na pia wataangalia uadilifu wako ndani ya taasisi yako hata ikiwa ndogo kiasi gani.

Hebu tuache ushabiki na unafiki. Kwa namna anavyoleta mabadiliko ya kuonekana katika klabu ya Yanga Afrika, leo hii Injinia Said Hersi akisimama jimboni na Lissu, kila mtu akatoa mifano ya namna anavyoweza kuleta mabadiliko ni nani atachaguliwa?

***Kwa maoni; 0768 888 787***



Mazingira

# ‘Kuna watu hawapikii gesi kwa sababu tu hawajazoea’

**Lakini nyumbani natumia gesi ambayo nanunua kwa Sh 25,000 nikiwa na familia ya watu sita tunatumia zaidi ya siku 30 kupika vyakula vingi isipokuwa kuchemsha maharage.**



**Na Lauden Mwambona, Mbozi**

KWA kuwa ni lazima watu wale, ni lazima pia chakula kipikwe majumbani. Kwa sasa kaya nyingi nchini hutumia aina nne za nishati kwa ajili ya kupikia.

Nishati hizo ni kuni, mkaa, umeme na gesi. Hapo nyuma nishati ya mafuta ya taa kwa maana ya matumizi ya majiko yale ya tambi au stovu ilikuwa pia inatumika. Lakini kwa sasa uchunguzi unaonesha kwamba, imekuwa ni nadra sana kuona majiko ya mafuta ya taa majumbani.

Watoto wengi wa siku hizi ukiwauliza kama wanajua kitu kinachoitwa stovu au tambi za jiko, watabaki wanashangaa. Wanajua tambi za kula!

Kwa nini matumizi ya nishati ya mafuta ya taa yamepungua sana majumbani ni suala linalohitaji uchunguzi lakini bila shaka hatua ya kupandisha bei ya mafuta hayo ili yasitumike kuchakachua dizeli ina mchango wake katika hilo.

Kwa mujibu wa Ofisa wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Kelvin Tarimo, asilimia 63.5 ya Watanzania wanatumia kuni kwa ajili ya kupikia, asilimia 26.2 wanatumia mkaa, asilimia tatu wanatumia gesi wakati wanaotumia umeme ni asilimia 2.2.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2019 kasi ya uharibifu wa misitu ni kubwa na kila mwaka zaidi ya hekta 469,420 zinaharibiwa kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.

Imekuwa ikielezwa kwa ukubwa huo wa misitu inayopotea kila mwaka ni sawa na ukubwa wa Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake.

Mbali na ukataji wa misitu kwa ajili ya kuni na mkaa, tafiti zilizopo zinaonesha kwamba kugeuza misitu kuwa mashamba sambamba na kilimo cha kuhamahama ndivyo vinamaliza zaidi misitu.

Shughuli nyingine za kibinadamu zinazomaliza misitu ni ufugaji wa makundi makubwa ya ng'ombe, ukataji wa misitu ya asili kwa ajili ya mbao na uchomaji moto misitu.

Serikali sasa imeshtuka kwani kama misitu itaendelea kufyekwa kwa sababu mbalimbali, moja ikiwa ni kwa ajili ya kuni na mkaa, Tanzania itageuka jangwa siku si nyingi. Tayari mikoa ya Kanda ya Kati na Ziwa imeanza kuonja athari ya kukosa misitu.

Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imetangaza mkakati wa kuwaelimisha Watanzania kuachana na nishati zisizo rafiki wa mazingira, hususan mkaa na kuni.

Rais Samia ameamua kuchukua hatua ya kuhamasisha matumizi ya majiko rafiki wa mazingira yakiwamo ya gesi. Kwa kuanzia, serikali imetoa fedha nyingi kulipia asilimia kadhaa ya gharama ya mitungi ya gesi ili iweze kuuzwa kwa Watanzania mbalimbali kwa bei nafuu.

Kwa mujibu wa taarifa ya viongozi wa REA, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/24 imeamua kutoa ruzuku kwa mitungi 2,700 kwa kila mkoa na tayari mitungi hiyo imeanza kuuzwa kwa bei ya punguzo.

Bei ya Mitungi hiyo inauzwa kwa kati ya Sh 20,000 na 23,000 badala ya Shilingi 45,000 hadi 50,000. Kampuni zilizopewa kazi ya kutoa mitungi ya bei punguzo ni za Oryx, O-gas, Taifa Gas na Lake Gas.

Wakati Watanzania wengi wakichangamkia mitungi ya bei poa, wapo wachache ambao wanasuasua kutumia gesi kwa maelezo kwamba gharama za uendeshaji ni kubwa. Wengi wanasema au wanahisi kwamba majiko ya gesi ni ya gharama zaidi kuliko mkaa ama kuni.

Lakini utafiti mdogo uliofanywa na mwandishi wa makala haya katika Kijiji cha Isangu kilicho kilometa tatu kutoka Vwawa mjini, wilaya ya Mbozi mkoani Songwe umeonesha kwamba wakazi wengi wa vijijini wanatumia gharama kubwa kwenye kuni na mkaa kuliko ambayo wangetumia gesi!

Kwamba, baada ya mtu kumiliki mtungi, gharama kubwa ziko wakati wa kujaza gesi ambako pesa nyingi zinahitajika lakini ukishakaza, gesi inakuwa gharama nafuu Dana kulinganisha na kuni au mkaa

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Abraham Nyingi anasema Kijiji kina kaya takribani 2,700. Hata hivyo, akasema hana uhakika na takwimu za wanaotumia majiko ya gesi ingawa wengi bado wanatumia mkaa na kuni.

Lakini kijana Meshack Msinjili anayeishi kwenye kijiji hicho na ambaye ana mke na mtoto mmoja, anasema yeye anatumia jiko la mkaa la jiko la gesi.

Hata hivyo, anasifia zaidi jiko la gesi akisema linatumika kwa usafi, linapika chakula kwa haraka na pia gharama za uendeshaji ni nafuu kuliko mkaa.

Msinjili anasema anapenda jiko la gesi kwa vile akijaza gesi kwa Sh 25,000 anatumia kwa miezi mitatu, lakini akinunua mkaa wa Sh 45,000 anatumia kwa miezi miwili tu.

Msinjili anasema ni vyema sasa vijana wajitofautishe kwa kuondokana na majiko ya kuni au mkaa badala yake anashauri wajielekeze katika kutumia majiko ya gesi au umeme.

Kwa mtazamo wake, mara nyingi matumizi ya mkaa na kuni ni mazoea tu au kudhani gesi na umeme ni ghali lakini vijana wengi na hata wazee wanawake kutumia nishati hiyo mbadala ya kupikia na kuachana na kuni na mkaa.

Anashauri vijana waipende miti kwani uwepo wake unasaidia katika kuvuta mvua, kuleta hewa safi ya oksijeni, kutunza vyanzo vya maji lakini kubwa ni kupambana na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kuleta athari lukuki katika dunia.

Pamoja na ushauri wake, bila shaka mtu anaweza kudhani kwamba Msinjili anasifia majiko ya gesi kwa sababu ana familia ndogo.

Lakini Fikiri Sampamba (39) wa Isangu, baba wa familia ya watu wanane, wanawe na ndugu, anazungumzia pia tofauti ya matumizi ya jiko la mkaa na la gesi katika uchumi.

Sampamba anasema mtungi wa gesi ananunua kwa Sh 25,000 na anatumia siku 20, lakini mkaa wa Sh 45,000 anatumia siku 30, jambo ambalo anaona gharama ni kubwa.

Mkazi huyo anataja kero ya mkaa kwamba ni pamoja na upatikanaji wake kuwa wa shida na kwamba pia ni moja ya vyanzo vya uchafu.

Fikiri ambaye ni mkulima, anafafanua zaidi kwamba matumizi ya gesi ni mazuri zaidi kwa vile yanajali usafi na wala hakuna moshi, lakini anaomba serikali isaidie kwenye punguzo la bei kujaza mtungi wa gesi.

Anasema urahisi wa mkaa au kuni upo kwenye kuweza kununua mkaa wa Sh 1,500 mpaka 2,000 kwa ajili ya matumizi ya siku, lakini kiasi hicho kwa mwezi ni zaidi ya Sh 40,000.

Naye mama lishe anayefanya kazi zake katika Mtaa wa Isangu, Vwawa, mkoani Songwe, Zepania Maega (41) anaona matumizi ya gesi yana tija kulinganisha na mkaa.

Mama lishe huyo maarufu kwa jina la Mama wawili, anasema katika mgahawa wake anatumia Sh 20,000 kila wiki kununua madebe manne ya mkaa ili aweze kupika wali, ugali, maharage, nyama na samaki.

“Lakini nyumbani natumia gesi ambayo nanunua kwa Sh 25,000 nikiwa na familia ya watu sita tunatumia zaidi ya siku 30 kupika vyakula vingi isipokuwa kuchemsha maharage,” anasema.

Mwanamke huyo anasema jiko la gesi ni la kistaarabu zaidi na anafikiria kuwa na mpango wa kuanza kutumia gesi hata kwenye mgahawa wake.

“Jiko la gesi linapika haraka, mikono wala nguo hazichafuki, na linadumu kama umelisimamia vizuri,” anasema.

Mama lishe huyo anasema changamoto ya mkaa ni pamoja na kusumbua kuwaka hasa ukilowa katika kipindi kama hiki cha mvua na pia kuuasha iko shughuli.

Kauli hiyo inaungwa mkono na muuza mkaa wa mafungu katika eneo la Isangu Sokoni aitwaye Christina Wega (25). Mwanamke huyo anasema kwa uzoefu wa kuuza mkaa miaka mitatu amegundua mkaa mwingine unasumbua sana kuwaka.

Waswahili wanasema safari ni hatua. Wakati wengine wanasuasua kuanza kutumia gesi kwa ajili ya kupikia, Rais Samia Suluhu Hassan anazidi kusisitiza haja ya kuwapunguzia kero za moshi jikoni wanawake nchini.

Anasema serikali inaangalia uwezekano wa kupunguza hata gharama za kujaza mtungi wa gesi baada ya kumalizika wa swali (wengine wanaita kubadilishabadilisha) ili upungue bei.

Bila shaka wakati umefika kwa kila Mtanzania kufanya mabadiliko hata ya kisaikolojia linapokuja suala nishati ya kupikia.

Watanzania hususan vijana hawana budi sasa kuwaza na kupenda kutumia majiko ya gesi na umeme kuliko kuendekeza majiko ya kizamani ya kuni na mkaa.

Ni hatua sahihi kwa Serikali kuanza kuchukua hatua za kuzuia matumizi ya kuni na mkaa kwenye taasisi zinazojumuisha watu wengi.

Wananchi pia tusisubiri na sisi kupewa ukomo wa matumizi ya mkaa na kuni. Tuanze sasa kubadilika kwani inaonekana kuna wanaoendelea au kuendekeza kutumia nishati hizo za tangu mababu na mababu si kwa sababu

# Maisha, maajabu ya mnyama sungura

**Na Godfrey Sanga kwa Msaada wa mtandao**

MNYAMA sungura ni miongoni mwa makundi ya mamalia wadogo waliomo katika familia ya Leporidae ya oda ya Lagomorpha na wanaopatikana sehemu mbalimbali za dunia.

Licha ya uzuri katika muonekano na utamu wa kutosha katika nyama yake, hutajwa kuwa miongoni mwa wanyama wajanja na wenye akili nyingi katika maisha yao.

### MAKAZI YAO

Licha ya kuenea duniani kote kwenye mazingira tofauti, sungura huishi sana kwenye maeneo yenye malisho ya majani, miti, misituni, vichakani na nyikani.

Pia huishi jangwani na sehemu tepe tepe.

### MAUMBO YAO

Wana masikio marefu karibu sentimeta 10 pengine ni mahususi kwa ajili ya kutambua adui. Wana miguu ya nyuma yenye nguvu, kila mguu una vidole vitano, huku kidole kimoja kikiwa kidogo mno kuliko vyote. Ukubwa wao ni takribani sentimita 20 mpaka 50 na uzito wa kilo 0.4 mpaka 2.

Manyoya yao huwa marefu na laini yenye rangi kati ya kahawia kijivu na manjano hafifu, mkia wao huwa mfupi uliojaa manyoya.

### TABIA

Kama wanyama wanaowindwa kwa ajili ya chakula hulazimika kuyachunguza kwa umakini mkubwa makazi yao mapya na pindi wanapopata vitisho au kuhisi hatari hutulia kimya na kutazama kwa makini.

Uoni wa sungura ni uwanja mpana na kwa kiasi kikubwa huweza hata kuona juu ya vichwa vyao hata akiwa ndani sungura atatafiti hali ya anga.

### UZAZI

Kawaida sungura jike hutegemea kujamiiana ili azae. Uterasi yao imegawanyika sehemu mbili, hivyo kupandana kunaweza kuhusisha matendo kadhaa ambayo yaweza kusababisha mimba kadhaa kutoka kwa madume tofauti.

Dume la sungura huwa hawawezi kutoa shahawa wakati wa joto la kiangazi (majira ya joto).

Sungura jike hubeba mimba kwa siku 30 mpaka 32 na huzaa watoto 12 hadi 13. Wakati mwingine huzaa watoto 18.

### CHAKULA

Sungura ni wanyama wala nyasi wanaokula hasa nyasi na majani ya magugu pia hula vinyesi vyao badala ya kuwa kama ng'ombe na wanyamma wengine ambao hula baada ya kucheua ili kumeng'enywa ili kupata virutubisho zaidi.

Sungura haraka sana kwa nusu saa ya kwanza ya malisho, mara nyingi mchana karibu na jioni, ikifuatia nusu saa nyingine ambapo hula kwa kuchagua sana chakula.



Ni wakati huu pia ndipo sungura atatoa kinyesi kigumu kama uchafu, ambacho yeye hatakila. Kama mazingira hayahatarishi, sungura atabaki nje kwa saa nyingi. Akiwa nje ya shimo lake, sungura hula kile jinyesi chake laini na hii huonwa mara chache zaidi, sababu hula tu baada ya kukitoa.

Kwa kawaida, sungura hutoa kinyesi chake kati ya saa mbili asubuhi na saa 11 na moja jioni akiwa ndani ya shimo lake.

Sungura pindi wanapowekwa ndani ya nyumba kwa ajili ya kufugwa, hutambulika kama sungura wa nyumbani.

Wakiwa ndani ya nyumba, sungura huwekwa kwenye sanduku lao kubwa lenye nafasi ya wao kutembea tembea.

Maeneo mengine sungura hufugwa maalumu kwa ajili ya nyama. Sungura huuawa kwa kugongwa kwa nguvu kisogoni kabla ya kuchinjwa.

Nyama ya sungura ni chanzo kizuri cha protini. Inaweza kutumiwa kw namna nyingi ambavyo nyama ya kuku ingeweza kutumika.

Kuna baadhi ya wapishi husema nyama ya sungura huwa na ladha ya kuku. Sungura pia ni chakula kizuri kwa chatu hasa kwa huko Bama ambapo chatu hula sungura mmoja kila baada ya wiki moja.

Ngozi ya sungura ikiwa na manyoya, hutumika nguo na mavazi mbalimbali kama vile kofia. Sungura waitwao angora hufugwa kwa ajili ya nywele zao ndefu zitumikazo kwa ajili ya nguo kama vile kondoo wa sufu.

Sungura pia huzalisha mbolea nzuri na mkojo wao wenye naitrojeni ya kutosha, hufanya milimao izae vizuri sana. Maziwa ya sungura pia huwa dawa na kirutubisho kizuri sana kwa sababu ya kiwango kikubwa cha protini.

### MATATIZO KWENYE MAZINGIRA


Sungura wamekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira pindi wanapowekwa kwenye mazingira mapya.

Kutokana na namna ya kula na kiwango chao kikubwa cha kuzaliana, sungura wa mwituni huwa chanzo kikubwa cha tatizo hasa kwenye kilimo.

### TAMADUNI

Sungura mara nyingi hutumika kama alama ya uzazi au kuzaliwa tena na mara nyingi wakihusishwa na Pasaka na majira ya kuchipua.

Na sungura kama mnyama anayewindwa tu (asiyewindwa), huwa alama nyingine ya Pasaka, kama alama ya mnyama asiyekosa.



## Dawati la Sheria

# Zijue sheria za kodi

**Na Sylivester Sebastian**

KAMA kuna mambo mawili ya uhakika ambayo kila aliyezaliwa na mwanamke hawezi kuyakwepa ni kifo na kodi. Ishi utakavyo huwezi kuepuka kifo na vilel vile hakuna anayeweza kuepuka kulipa kodi.

Zipo kodi ambazo mtu analipa moja kwa moja (direct taxes) lakini zipo kodi zinazolipwa kupitia manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimabli (indirect taxes).

Kodi ni msingi wa ustawi wa taifa lolote duniani. Hakuna serikali yenye shamba au biashara kwa ajili ya mapato yake isipokuwa serikali zote duniani hutegemea mapato yake ya uhakika kupitia kodi.

Jinsi mahitaji ya jamii yanavyoongezeka ndivyo kiwango na wigo wa kodi kinavyoongezeka pia. Kwa hiyo ni wazi kwamba maisha ya kila mwanadamu yanashikmanana kulipa kodi kwa serikali.

Makala hii inafafanua sheria mbali mbali za kodi ambazo zimetungwa na zinatumika ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo ni kuongeza uelewa kwa watanzania na wageni kuhusu sheria za kodi zinazotumika hapa nchini.

Ufahamu wa sheria za kodi unarahisisha uanzishaji na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. Aidha, uelewa mpana wa sheria hizi husaidia uwepo wa utii wa sheria, upungufu wa migogoro ya kikodi na huleta usitawi jamii na ukuwaji wa uchumi kwa ujumla. tukumbuke kuwa Tanzania inazo sheria, kanuni na mingozo mbali mbali inayoanzisha aina mbali mbali za kodi na taratibu za ulipaji na usimamizi wa kodi.

Makala hii l inachambua kwa kina sheria, taratibu, kanuni na miongozo iliyowekwa katika ulipaji na usimamizi wa masuala ya kodi nchini.

**MAANA YA KODI**

Kwa ufupi, kodi inaweza kuelezwa kama michango ya lazima iliyowekwa kwa mujibu wa sheria ambayo huwasilishwa serikalini ili kuiwezesha serikali hiyo kujiendesha na kutoa huduma za kijamii kwa wananchi.

Michango hiyo inaweza kuwa inatolewa kwa utaratibu wa kutegmemea kipato cha mtu, matumizi yake ya kila siku, mali, mwenendo wa maisha na kadhalika.

**MSINGI WA KODI**

Kwa nchi zinazofuata utawala wa sheria, msingi wa kodi upo kwenye sheria zinazotungwa na mamlaka zilizowekwa kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kazi hiyo. Msingi wa kodi hapa nchini umejenjwa kwenye sheria mbali mbali ikiwa ni pamoja na Ibara ya 138 (1) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muugana wa Tanzania ya 1977 inayoeleza wazi kuwa hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu kisheria na sheria iliyotungwa na Bunge.

Ibara ya 99 inatamka kwamba Bunge linaweza kutunga au kubadili sheria inayoanzisha kodi au kubadilisha kiwango cha kodi cha juu zaidi pale ambapo litakuwa limeelekezwa kufanya hivyo na Rais wa nchi. Hivyo sheria zote, kanuni, taratibu na miongozo kuhusiana na masuala ya kodi, upata

Baraka zake kutoka kwenye katiba ya nchi kama ilivyoelezwa.

**MADHUMUNI YA KODI**

Kodi huanzishwa kwa madhumuni kadha wa kadha kulingana na malengo ya Serikali na mahitaji ya jamii husika. Baadhi ya madhumini ya kuanzishwa kwa kodi mablimabli ni kama haya yafuatayo;

> **Kutokana na kodi, serikali huanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji au utoaji wa uduma ambazo mwisho wa siku huchochea ukuaji wa kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa...**

Uhitaji wa mapato Kama ilivyoolezwa awali, watu hutegemea serilikali yao kuwapatia baadhi ya mahitaji muhimu katika uendeshaji wa maisha. Lakini Serikali haina shamba. Hivyo serikali nayo hutegemea wananchi wake kulipa kodi ili ipate kipato cha kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Kwa lugha nyingine, uhitaji wa nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma, kwa mfano, unaweza kupelekea kupandishwa kwa viwango vya kodi au uwazishwaji wa kodi mpya ili kufanikisha lengo hilo.

Ili Serikali iweze kumudu kujiendesha na kutimiza matakwa ya wananchi wake ni lazima izingatie pamoja na mambo mengine, ulipaji wa kodi. Kwa mantiki hiyo madhumuni ya kodi ni uhitaji wa mapato kwa serikali kwa wakati husika.

Uhitaji wa mtaji kwa ajili ya uwekezaji Uchumi wa nchi hutegemea kwa kiwango kikubwa uwekezaji unaofanywa na Serikali katika jitiahada za upatikanaji wa kipato kwa ajili ya utoaji wa huduma

kwa wananchi.

Hivyo kodi huweza kuanzishwa kwa ajili ya kukusanya mtaji na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi ili kuzalisha zaidi na kukuza uchumi wa nchi.

Kutokana na kodi, serikali huanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji au utoaji wa uduma ambazo mwisho wa siku huchochea ukuaji wa kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Mifano halisi ni kama; ujenzi wa miundombinu ya barabara, bwawa la kuzalisha umeme, uboreshaji wa bandari, ujenzi wa reli, hospitali na kadhalika.

Ulizi wa bidhaa za ndani

Baadhi ya kodi huanzishwa na sheria kwa ajili tu ya bidhaa au huduma zinazotoka nje ya nchi. Lengo la kuanzishwa kwake ni kuweka ugumu kwa waingizaji wa bidhaa hizo ndani ya nchi ambazo hulenga kuua soko la ndani.

Kwa maana nyingine ni kuwa uwepo wa kodi hizo huwafanya waingizaji wa bidhaa kushindwa kushindana na wazalishaji wa ndani na hivyo kukata tamaa. Mwisho wa siku, uzalishaji wa ndani hukua kutokana na kulindwa kupitia kodi.

Kuzuia ungizwaji holela wa bidhaa chakavu Kuna aina za kodi zinazoanzishwa kwa ajili ya kuzuia au kupunguza uingizwaji nchini wa bidhaa ambazo ni hatarishi au chakavu.

Mfano halisi wa hilo ni kodi iliyowekwa kwa magari ya mitumba ambayo yameshakaa muda mrefu tangu kuundwa kwake au aina fulani ya nguo za za mitumba.

**AINA ZA KODI ZINAZOLIPWA TANZANIA,**

Sheria za Kodi Tanzania zimeanzisha kodi za aina mbalimbali. Baadhi ya kodi hizo ni kodi ya mapato ya watu binafsi, kodi ya makampuni, kodi ya mapato yatokanayo na ajira na kodi ya uendelezaji ufundi stadi (SDL).

Aina nyingine ya kodi ni kodi ya zuio, kodi yan mapato ya uwekezaji raslimali, kodi ya ongezeko la thamani, ushuru wa bidhaa, ushuru wa stempu, kodi ya matumizi ya barabara, kodi katika michezo ya kubahatisha na kadhalika.

**SHERIA ZA KODI TANZANIA**

Kama ilivyoelezwa awali, kodi zote huanzishwa kwa sheria. Tanzania inazo sheria mama za kodi pamoja na kanuni mbali mbali zinazolenga kufafanua ulipaji na usiamamizi wa kodi nchini.

Baadhi ya sheria mama zinazoanzisha na kutoa mwongozo wa uratibu na usimamizi wa kodi ni kamaifuatavyo; Katiba ya Jamuri ya Muungano wa Tanzania, 1977; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura Na. 438; Sheria ya Kodi ya Mapato Sura Na.332;

Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura Na. 148; Sheria ya Malipo ya Uduma ya Bandari Sura Na. 264 na Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Umiliki wa Magari Sura Na.124; Nyingine ni Sheria ya Malipo ya huduma kwenye viwanja vya ndege, ,Sura Na.365; Sheria ya Ushuru wa barabara Sura Na. 220; Sheria ya Stempu, Sura Na.189; Sheria ya Afrika Mashariki kuhusu Usimamizi wa Forodha, toleo la 2011;Sheria ya Afrika Mashariki kuhusu Usimamizi wa Vituo utoji wa huduma za bandari kwa pamoja, toleo la 2016 na Sheria ya Michezo ya bahati na sibu Sura Na. 41;

Sheria nyinginezinazoanzisha na kutoa mwongozo wa uratibu na usimamizi wa kodi ni Sheria ya Ushuru wa Magari yaendayo nje ya nchi Sura Na.84; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura Na. 147; Sheria ya Ushuru na Usimamzia wa Forodha Sura Na. 403; Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki Toleo la 2017; Sheria ya Elimu na Ufundi Sura Na. 82, n.k.

Wiki ijayo tutaanza kutoa ufafanuzi kuhusu aina mbalimbali za Kodi pamoja sheria zake.

**Inaendelea...**



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Mambo ambayo watu wenye nguvu ya akili hawayafanyi -1

YAPO mambo ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili hawayafanyi kwenye maisha yao. Na hatua yao ya kuyaacha mambo hayo ndiyo inasababisha wasonge mbele kwa haraka.

Bahati mbaya iliyopo ni kwamba watu wenye nguvu ya kuyaacha haya ni wachache kwenye jamii zetu. Wengi wanashindwa kuyaacha mambo haya na kujikuta wakiendelea kuishi maisha ya chini siku zote.

Katika kliniki yetu ya leo, ninayaeleza hayo mambo japo kwa kifupi ili ujitahidi kuyafanyia kazi. Nayo ni kama ifuatavyo:-

### HAWAPOTEZI MUDA KUJIONEA HURUMA

Watu wote katika maisha, hupata maumivu na huzuni kwa sababu maisha ya mabonde na milima. Watu wanapitia sintofahamu nyingi na wakati mwingine kufanyiwa matendo yasiyo ya kiungwana, dharau au kudhulumiwa.

Mambo haya huwafanya watu wengi kubakia hapo walipo na kupoteza muda mwingi wakijionea huruma na kuwaza mambo ambayo huzalisha huzuni na maumivu maishani mwao.

Mtu dhaifu baada ya kupitia madhila makubwa hujikuta na mawazo mengi hasi. Mfano, hujiona kama yeye ndiye mwenye matatizo kuliko watu wengine duniani, huona kama Mwenyezi Mungu amemtupa, ana mikosi na mengine mfano wa hayo. Fikra za aina hii zinaua ujasiri, ubunifu na nguvu.

Ni fikra ambazo huchochea hisia za kutojiamini na kujiona duni mbele ya wengine. Mambo haya kamwe ukiyatilia maanani hayakupi nafasi ya kufanikiwa sababu ili mtu afanikiwe, msingi ni kujiamini na kuwa jasiri sababu vita lazima uishinde kwanza ndani.

Mitihani ya maisha ambayo mtu anapitia, inapaswa kuwa chachu ya mara mbilimbili katika kutafuta njia ya kutokea badala ya kukaa akiendelea kugugumia maumivu kila kukicha.

Kinyume chake, watu wenye nguvu ya akili huepuka kabisa kukumbatia maumivu na huzuni muda wote. Hawakai wakiendelea kujionea huruma

tamaa lililokukuta, ukichunguza kuna wengine yamewakuta makubwa zaidi na hivyo hilo lako ni 'cha mtoto'.

Tafadhali, kama unawaza mafanikio, imarisha nguvu ya akili yako katika kushinda tabia hii ya kukumbatia maumivu, huzuni na kujionea huruma.

maadui. Kwa kufanya hivyo, tunakuwa tunawapa nguvu zetu. Wanachukua akili chanya yenye nguvu ndani yetu na kuzalisha hasia na fikra za kutamani visasi.

Wanachukua usingizi wetu, amani yetu, hamu yetu ya kufanya mambo na matokeo yake wanatupa mzio (stress) na mashinikizo ya damu.



au kutafuta kuonewa huruma kwa sababu matokeo yake ni kupoteza muda, kuzalisha hisia hasi, kujitabiria unyonge, kushindwa, kukusahaulisha kabisawema mkubwa wa Mungu kwenye maisha yako na kukufanya kuwa mwathirika wa kisaikolojia (depression), jambo ambalo si tabia ya kuvutia mafanikio.

### NGUVU ZAO HAWAWAPI WENGINE

Nikisema kwamba watu wenye nguvu ya akili hawatoi nguvu zao kuwapa wengine, inaweza kuwa ngumu kueleweka. Lakini ni kwamba tunapokaa na vitu mioyoni vinavyotudhuru na kuchukua eneo kubwa la nguvu zetu za kufikiri, tunawapa watu wengine nguvu zetu.

Vitu hivyo ni kama kukaa

Hasira na chuki vinamwondoa mtu kwenye njia na kumbadilishia mtazamo

wake wa namna ya kufikiria, kuhisi na kadhalika. Watu wenye nguvu ya akili hawafanyi kazi haya. Vinapokuja vitu vya kuwaondoa njia kuu wanavidharau na kusamehe na kisha kusonga mbele. Kwa kufanya hivi wanabaki na nguvu

### KUFANYA MABADILIKO CHANYA

Kwenye hii dunia si kwamb wengine wana utashi sana n wengine hawana ila ni kwamb baadhi ya watu wana utayari w haraka wa kubadilika na wengin hawako tayari (au ni wagumu kubadilika.

Mara nyingi ni rahisi kusem unataka kubadilika lakin kiuhalisia mabadiliko ni jamb gumu na wanaoliweza ni wal tu wenye nguvu kubwa ya aki ambao hujenga nguvu kubwa y maamuzi. Mawazo na hisia zet mara nyingi hutuzuia kutekelez mabadiliko hasa ya kitabi kuelekea mafanikio yetu.

Mfano, kama umezoe ratiba fulani ni ngumu kuiach ratiba hiyo na kubadilika. Le kuhusu kufanya mazoezi, weng wanapenda lakini kubadilik kuielekea ratiba hiyo siyo rahis Leo kuhusu suala la kuwa n ratiba za kumwomba Mungu n kusoma Neno la Mungu wat wanapenda lakini kubadilik kuelekea huko ni ngumu.

Ukiwaambia watu kuwa jamb la kwanza baada ya kupata fedh yoyote ni kuweka akiba kwanz kabla ya kufikiria ya kutumia kila mmoja anapenda lakin kubadilika kuelekea huko s jambo dogo.

Sasa hapa ndipo weny nguvu ya akili wanapotuzid hawachelewi kubadilika. Mar nyingi kubadilika kunafuat mtiririko wa hatua tanc Hatua hizo ya kwanza 'wazo (Precontemplation), yaan mawazo yanayoleta uhitaji w mabadiliko na pili ni 'tafakur (contemplation) ambapo hap mtu huanza kutafakari faid za kubadilika na hasara z kutobadilika.

Jambo la tatu katik mtiririko huo ni 'maandaliz (preparations). Hii ni hatu ambayo mtu huja na mpang unaoainisha hatua madhubu zinazotambulisha kil anachoenda kukifanya tofauti n awali.

Jambo la nne ni 'kutendea kaz (action). Hapa mabadiliko halis ya kitabia huanza kuonekana Hatua ya tano katika mtiririk wa mabadiliko ni kudumish mabadiliko (maintenance) Katika hatua hii mtu hupingan na vikwazo vinavyoinuk kumrudisha kwenye hali y kawaida, yaani kule anakotoka.

Your Partner in Growth.



Na Hamisi Kibari
Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 7

**CHRIS baada ya kunogewa na penzi la Joyce, Miss Tabora wa zamani, anatelekeza familia. Mkewe anapoamua kwenda kwao kulalamika, Chris anahamia nyumbani kwake na hawara yake huyo ili kupunguza gharama za kuishi hoteli. Mkewe anaporejea ghafla kunatokea mtafaruku baina ya mkewe na hawara, hali inayosababisha mfanyabiashara huyo anayeendesha duka kubwa la mbao ampige mkewe hadi kuzirai. Anampeleka mkewe hospitalini na kurejea nyumbani lakini wakati akijiandaa kumpeleka mwanae Huba kwa dada yake, anapata ugeni... Nini kitatokea?**

"Kwa jinsi anavyompenda Mama Kenny nitaanza kwa kudai ninataka kubadilika, niachane na Joy kwa afya ya ndoa yangu. Halafu nitamweleza kilichotokea nikijifanya kimenigusa sana. Atanielewa," alijisemea.

Wakati anakaribia mlango wa kutoka nje akiwa amemshika mwanawe, hodi ikasikika.

Chris, akasita kidogo akisikilizia. Hodi ikagongwa tena. Kwa kuwa alikuwa karibu na mlango, akapiga hatua chache, akanyoosha mkono na kufungua mlango. Akakutana mlangoni na dada yake, Mwalimu Misango akiwa ameandamana na kaka yake Mama Kenny, Jacob pamoja na baba mkwe wake.

Akasikia moyo unafanya pa.

Akakumbuka maneno ya mkewe kabla ya kutokea ugomvi usiku ule. "Nitoke niende wapi… Kama hun'taki hilo ni suala jingine. Hapa ni kwangu. Wazazi wangu wanakuja kesho kutwa tuongee haya mambo. Hapo ndipo nitajua kuondoka kama kweli hunitaki. Kwetu sijafukuzwa. Nilitokea mlangoni, sikupitia dirishani miye."

Kwa sekunde kadhaa Chris alibaki akiwaangalia wale wageni mlangoni akiwa kama ameganda. Huku akihisi hali ya wasiwasi. Mkewe alikuwa amesema wazazi wake wangekuja keshekutwa, kwa maana siku iliyokuwa inafuata.

"Kwa nini wamekuja sasa?" Alijiuliza.

Aliwatolea salamu na kuwakaribisha ndani. Wakaingia.

"Baba Kenny, hawa ni wageni wako, wamekuja kuongelea tatizo lako na mkeo. Ilikuwa waje kesho lakini kuna dharura fulani ya shemeji yako, kesho hatokuwepo. Wakaona waje sasa hivi. Mbaya zaidi simu ya mkeo haipatikani na ya kwako hupokei," alisema Mama Kessy au Mwalimu Misango kama alivyofahamika zaidi kwa wengi.

"Baba na shemeji karibuni sana. Lakini ninaomba mtanisamehe angalau kwa leo kwa sababu nina haraka kidogo. Ilikuwa nipitie kwa dada kumpeleka huyu Huba kwani kuna wafanyabiashara fulani wenzangu wametoka mbali wananisubiri ofisini. Na nimeshawachelewesha sana. Wakiondoka bila kuonana nao nitapata hasara kubwa sana. Mtanisamehe kwa sasa. Hiki kikao tukipangie muda mwingine."

"Umpitishe kwangu mtoto, kwani mama yake yuko wapi?... Hebu kaa chini kidogo Baba Kenny utusikilize. Hata sisi wote hapa tuna haraka na tumeacha shughuli zetu muhimu vilevile. Mzee amefunga safari kuja huku kalipa nauli... Hebu acha ufedhuli, Chris," alisema Mwalimu Misango kwa sauti ya mamlaka.

"Itakuwa vigumu dada kwa sasa. Samahani sana. Lazima niwahi. Hata hivyo, tutaongea baadaye. Kama shemeji hatokuwepo kesho bora tufanye leo jioni" alijibu Chris ambaye alijiona hana majibu tayari kuhusu mkewe. Hakuwa na hakika kama ikifika hiyo jioni atakuwa na majibu na hivyo alipanga akiona hana cha kusema bado atatafuta namna ya kutokutana nao.

Wakati Mwalimu Misango akitaka kufunga mdomo kujibu hoja ya mdogo wake iliyoonekana kumshangaza kila aliyekuwepo mahala pale, hodi ikasikika.

Kwa kuwa mlango wa kuingia sebuleni kutokea nje ulikuwa wazi, mgongaji hakusubiri, bali alifungua mlango na hivyo alikuwa mwenyeji.

Mwalimu Misango na wageni alioandamana nao walihisi huyo anaweza kuwa Mama Kenny, lakini kwa mshangao akaingia mtu mwingine. Alikuwa Joyce. Ujio ule ulionekana kumchanganya hata Chris ambaye alitamani kumzuia kuingia. Kila mmoja akamkodolea macho msicha yule mrembo akitembea kwa madaha.

"Chris, nashukuru nimekuwahi. Kwa vile naona una wageni niko chumbani ninakusubiri. Nadhani hakuna mtu (huko chumbani)," alisema Joyce baada ya kutoa salamu ya jumla.

Hakusubiri majibu akaanza kupiga hatua kuelekea chumbani kwa Chris huku Mwalimu Misango akishangaa na Chris akiendelea kuhisi kutaka kuchanganyikiwa kutokana na ujio ule.

"Lakini baba Kenny, kama nilivyosema mkweo kafunga safari hadi huku kwa ajili ya maongezi haya na anatakiwa arudi haraka kuendelea na shughuli zake. Kesho shemeji yako ana dharura. Naomba ujitahidi tuyaongee haraka haraka haraka," anasema Mwalimu Misango.

"Kwani kuna tatizo gani kubwa dada? Kwanza Mama Kenny hayupo... Baba yeye angerudi tu nyumbani kama ana haraka. Shemeji pia hana sababu ya kuacha shughuli zake. Haya ni mambo madogo tu."

> **Umpitishe kwangu mtoto, kwani mama yake yuko wapi?... Hebu kaa chini kidogo Baba Kenny utusikilize. Hata sisi wote hapa tuna haraka na tumeacha shughuli zetu muhimu vilevile. Mzee amefunga safari kuja huku kalipa nauli... Hebu acha ufedhuli, Chris.**

"Nipe namba ya simu ya hao watu niongee nao. Nitawaomba radhi mimi kwa niaba yako," alisema Mwalimu Misango akishikilia simu yake tayari kuandika namba. "Kimsingi kila mtu hapa ameshasikia malalamiko ya mkeo, hata kama hatokuwepo. Hatujasikia upande wako."

"Ebo! Mbona sikuelewi dada. Wewe ndiye mwenye haraka au baba na shemeji? Nina hakika kikao hiki tunaweza kukiahirisha hadi jioni."

Kauli ile ilimfanya baba mkwe wake aingilie kati: "Samahani mkwe. Mimi siku moja nilimwona mkeo nyumbani nikadhani kaja kutusalimu. Nilipomuuliza ananiambia huku kuna matatizo. Nikamuuliza 'mumeo kakuruhusu na kakupa barua uniletee?' Yeye aliniambia kaja tu hata wewe huna habari. Ndio maana nimemrudisha na nikaamua kuja mwenyewe nisikilize hasa kwa nini alikuja nyumbani kwangu bila ruhusa yako. Ni kinyume na utamaduni wetu. Ni jambo dogo tu mwanangu."

"Ni kweli mzee. Mama Kenny alikuja huko mimi nikiwa sina habari na hata sasa kwa kweli sijui yuko wapi. Kaja jana kabwaga mtoto hapa na kuondoka… Lakini haya matatizo nitayamaliza tu."

"Ebo! Hujui mkeo yuko wapi? Au kaondoka baada ya kukuta umemletea hawara chumbani mwake... Yaani sijui nani kakuroga mdogo wangu," akamaka Mwalimu Misango.

"Mimi sijui kaenda wapi. Alibwaga mtoto usiku akatokomea anapopajua. Ndio maana nilitaka nimlete Huba kwako," alilazimika kuongopa.

"Atakuwa ameenda wapi sasa, kwa sababu kwangu pia hajafika na kwa wifi yake hayupo," alihoji Jacob, kaka wa Mama Kenny, kwa maana ya mtoto wa baba yake mkubwa aliyekuwa anafanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

"Kwanza ni ajabu aamue kutoka hapa na kwenda sehemu bila kupitia kwangu. Nini kimetokea?" Akahoji Mwalimu Misango akionesha mshangao.

"Ni kama nilivyosema. Alibwaga mtoto akaondoka zake," Chris akazidi kuongopa.

Mzee Chitawo, Baba yake Mama Kenny alimgeukia Chris baada ya kimya kifupi kupita: "Sasa baba, wewe unahisi huyu mwenzio yuko wapi?"

"Kwa kweli sijui mahala aliko, baba. Niliposema nina haraka ndio nilikuwa ninataka nikutane na wale wafanyabiashara wenzangu na kisha nianze mara moja juhudi za kumsaka... Lakini nina hakika nitampata tu," akajibu Chris.

"Isije ikawa kajinyonga. Ninamjua yule roho yake nyepesi anapokuwa na matatizo," alisema Jacob, ambaye alikulia kwa baba yake mdogo, yaani kwao Mama Kenny.

"Bwana Shemeji, hapa hakuna tatizo kubwa la mtu kufikia hatua ya kujinyonga. Mimi ninahisi yupo mahala tu kabana."

"Kinachonishangaza anajua ugeni huu hata kama mpango ulikuwa ni kuja hapa kesho. Tulikuja wote, mimi nikaenda kulala kwa shemeji yako Jacob na yeye akaja huku. Sasa imekuwaje abwage mtoto na kutoka?"

"Mzee sababu inajulikana. Huyu bwanamdogo hataki tu kunyoosha maneno. Sababu ni huyo mwanamke aliyetupita hapa na kwenda chumbani kwa Mama Kenny. Mwanamke gani anaweza kukubali kufanyiwa ushenzi kama huu. Hapa kuna mawili; ama huyu bwanamdogo kamfukuza au yamemshinda na kuamua kuondoka."

"Sasa ni wapi kaenda? Hajaja kwako wala kwa kaka yake," akahoji Mzee Chitawo.

"Hata mimi sijui... Jamani nina haraka. Nina jukumu pia la kumtafuta Mama Kenny kama nilivyokwisha sema. Kuendelea kulumbana hapa haisadii lolote," alisema Chris akinyanyuka.

"Haya baba wewe nenda ukamtafute mwenzio... Kwa hiyo tutakutana jioni au kesho?" Akahoji Mzee Chitawo.

"Baba wewe ungerudi tu nyumbani uendelee na majukumu mengine. Kuna tatizo dogo tu hapa mimi na mke wangu tutalimaliza tu. Wala sina wasiwasi."

Mwalimu Misango akaingilia kati: "Hapana. Tatizo si dogo. Nadhani kilichomleta mzee ni kushindwa kujua sababu zilizomfanya aende kwao bila idhini yako mumewe uliyemtolea mahari. Hizi ni zama za uwazi na ukweli, hivyo ni vyema mambo yote yakawa hadharani pengine ikasaidia kuwekana sawa. Sote tuna lengo moja na zuri, kuona ndoa yenu nzuri inaendelea kusimama. Basi mama Kenny atafutwe tufanye kikao jioni."

Chris akaitikia kwa kichwa.

***

Chris alifungua mlango wa chumba cha daktari kama mtu aliyefukuzwa. Uso wake ulikuwa na mashaka makubwa. Kijasho chembamba kilikuwa bado kinamtoka, kitiririka hadi makwapani. Mdomo wake ulikuwa umemkauka ghafla kwa kupoteza maji. Njiani alinusurika mara mbili kugongwa na gari kwa jinsi alivyokuwa amechanganyikiwa.

Daktari alimkaribisha: "Karibu Mr. Magati. Umejitahidi kuchunga muda kwa sababu baada ya nusu saa tutakuwa na kikao."

"Ndugu yangu, toka nilipopata simu yako nimechanganyikiwa. Sijui utanisaidiaje kuhusu hili. Ni kweli ulichoniambia?"

"Kaza moyo ndugu yangu. Ninafahamu jinsi ilivyo ngumu kuamini."

*Itaendelea*

## VITA VYA ISRAEL, HAMAS:

# Netanyahu: Israel itakuwa na jukumu la usalama kwa Gaza

**YERUSALEM, Israel**

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema nchi yake itakuwa na jukumu la jumla la usalama kwa Ukanda wa Gaza kwa kwa muda usiojulikana mara baada ya mapigano yatakapomalizika,

Netanyahu alitoa kauli hiyo katika mahojiano na kituo cha Marekani cha ABC News, ambapo pia alitupilia mbali wito wa kusitishwa kwa mapigano bila ya kuachiliwa kwa mateka waliochukuliwa na Hamas katika mashambulizi yao ya Oktoba 7, mwaka huu. Hata hivyo, alisema kusitishwa kwa misaada ya kibinadamu, huenda itawezekana.

Kuhusu kusitishwa kwa vita kidogo kimkakati - saa moja hapa, saa moja pale - tumekuwa nayo awali. Nadhani tutaangalia mazingira ili kuwezesha bidhaa na misaada ya kibinadamu kuingia, au mateka wetu na mateka wa kibinafsi kuondoka, alisema Netanyahu.





# Ukraine yategemea kupata uanachama EU

**KYIV, Ukraine**



UKRAINE inatarajia kupokea mwitikio mzuri kutoka Umoja wa Ulaya (EU) kwa maendeleo yake ya kupata uanachama, Naibu Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Olha Stefanishyna, ameiambia Reuters, mwanzoni mwa wiki hii.

Stefanishyna alisema Kyiv, imetekeleza mageuzi yote yaliyohitajika. Inatarajia ripoti ya Jumatano ijayo itatoa ishara ya mwanzo wa mazungumzo ya Ukraine kuingia EU kuanzia Desemba, mwaka huu. Uanachama wa EU unachukua miaka mingi kuupata, ambapo mwombaji anatakiwa akamilishe vigezo vikali vya kisheria na kiuchumi kabla ya kujiunga. EU ambayo ina nchi wanachama 27, haipo tayari kutoa uanachama kwa nchi iliyopo vitani.

Poland, ambayo ni mwanachama wa EU, waendesha malori wake walifunga mipaka mitatu na Ukraine, Jumatatu, wakipinga kushindwa kwa serekali kulinda biashara kutokana na ushindani wa wageni tangu kuanza kwa uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

DW.

# Balozi wa Ufaransa UN atoa wito wa kusitishwa mapigano




**NEY YORK, Marekani**

BALOZI wa Ufaransa katika Umoja wa Mataifa (UN), ametoa wito wa kuwepo kwa maafikiano ya kibinadamu huko Gaza.

Kufuatia kikao cha Baraza la Usalama kilichokuwa cha faragha, Balozi Nicolas De Rivière, alisema mapatano hayo yanapaswa kudumu na kuwezesha kusitishwa kwa mapigano.

Msimamo huo unaonekana kutofautiana na washirika wengine wa Magharibi kama vile Marekani na Uingereza, ambao wanasema usitishaji wa mapigano ungefaidi Hamas pekee.

Mapema Jumatatu, John Kirby, Msemaji wa Usalama wa Kitaifa wa Marekani, alisema nchi yake haiamini kwamba usitishaji vita wa jumla, ulikuwa unafaa kwa wakati huu.

De Rivière pia alisema kuwa Ufaransa itakuwa mwenyeji wa mkutano wa kibinadamu huko Paris kesho Alhamisi katika juhudi za kupata msaada wa ziada kwa Gaza.

# Fedha na Majungu ziliua Empire Bakuba

**KAMA tulivyoahidi wiki iliyopita, wiki hii tutaanza mfululizo wa makala za baadhi ya waliokuwa wanamuziki wa bendi ya Empire Bakuba iliyokuwa ikiiongozwa na Pepe Kalle. Mwandishi Wetu PETTER MWENDAPOLE amezungumza na Djouna Mombafu maarufu kama 'Bileku Mpasi' endelea:**

MOJA ya bendi kubwa zilizowahi kutingisha Afrika ni Empire Bakuba. Bendi hii ilikuwa ikiongozwa na Tembo wa Afrika, Kabasele Yampanya maarufu kama Pepe Kalle.

Kati ya vivutio vikubwa kwenye bendi hii ilikuwa Pepe Kalle mwenyewe, mchezaji mshoo mfupi kabisa Emolo na repa mwenye vituko, Bileku Mpasi, muunganiko huu pamoja na waimbaji kama Dilu Dilomona, Papy Tex Matolu mpiga bass aliyekuwa mdogo sana wakati huo Gode Lofombo na mpiga solo Elvis Kunku ilikuwa burudani nzuri.

Lakini pamoja na nyimbo nyingi nzuri kama Young Afrika, Roger Miller, Mpenzi Bupe, Hidaya, Mamie, Full Option, bendi ilivunjika muda mfupi baada ya kifo cha mwasisi wake Pepe Kalle aliyefariki Oktoba 28 mwaka 1998.

Katika mazungumzo na safu hii, Bileku anasema kutoaminiana na wivu ndio ulisambaratisha Empire Bakuba na kufanya wanamuziki wengine kujitoa na wengine kubaki.

"Empire Bakuba haijafa kama wengi wanavyodhani lakini iligawanyika...na hii imeacha upande mmoja una nguvu na mwingine ukiwa hauna nguvu pamoja na kujitahidi kutoa albamu tangu wakati huo.

"Wakati Mzee anafariki, mimi ndio nilikuwa kiongozi wa bendi... Nilipewa uongozi wa bendi kutokana na uwezo wangu, lakini ile hali ya ukaribu na Mzee Pepe ikaonekana mimi na Emoro (Tumba Ayira) tunapendelewa," anasema.

Katika mazungumzo haya, Bileku muda wote alikuwa akimtaja Pepe Kalle kama Mzee. Anasema baada ya kifo cha Pepe Kalle, hakuwa na thamani tena ndani ya bendi ya Empire Bakuba, na hakuwa na kauli yoyote tofauti na enzi za uhai wa mwenye mali.

"Kiliitishwa kikao huku kukiwa na hisia kuwa alikuwa ameachiwa hela nyingi sana, lakini ukweli hakukuwa hata na shilingi moja niliyoachiwa, sikuwa na kauli na ukweli waanzilishi Mzee Dilu Dilomona na Papy Tex walikuwepo. Haya Mzee alitabiri kabla ya kifo chake kwamba, ikitokea ameondoka wenzake watanisumbua sana," anasema.



Baada ya kikao kuona hakieleweki, Lofombo alisimama na kueleza kuwa yeye anajitoa kwenye bendi na atafanya shughuli zake binafsi za muziki na endapo Bakuba watamuhitaji basi atawasaidia.

Anasema hakukuwa na maelewano tena na kila mmoja akachukua njia zake.

"Baada ya kikao Lofombo alinifuata na kunieleza sisi bado vijana twende tukapige kazi, tukawaachia wazee Dilu pamoja na Papy Tex bendi... nilifuata nae lakini tayari kichwani nilikuwa na mipango yangu, baada ya muda nikaenda njia yangu," Anasema.

**Baada ya kikao Lofombo alinifuata na kunieleza sisi bado vijana twende tukapige kazi, tukawaachia wazee Dilu pamoja na Papy Tex bendi...nilifuata nae lakini tayari kichwani nilikuwa...**

Anasema hapo ndio alianzisha bendi yake ya Big One Music ikiwa na makao yake makuu Kinshasa Kongo akiwa na vijana Chipukizi 12 lakini akiwa yeye mwenyewe anaishi nchini Uingereza na kufanya maonyesho mengi nchini humo.

Bileku anasema mpaka sasa bendi hiyo imetoa albamu moja inayofahamika kwa jina la Tonnerre De Brest iliyofanya vizuri na kuweza kuingia kwenye tuzo za muziki Black Music nchini Benin.

Albamu hiyo ilimpa mafanikio mengine ikiwa ni pamoja kupata mwaliko wa Rais wa Guinea, kabla ya kupata mkataba wa kutumbuiza Angola na kupewa mkataba nchini Kongo na kampuni ya Bia Bralima yeye akitangaza bia ya Turbo King.



Wanamuziki waandamizi wa Em.pire Bakuba, Kutoka kushoto ni Dilu Dilumona, Bileku Mpasi' Pepe Kalle na mbele ni Emoro





Mpiga Bass, Gode Lofombo

Turbo ilimzungusha Kongo nzima na baadae kutoka kwenda Zimbabwe maonyesho sita. Baada ya hapo aliitwa na serikali ya Angola baadae Canada.

"Niliitwa tena Angola katika mkoa wa Banza Kongo nikapiga shoo na kufuatiwa na nyingine ya VIP, Serena tukiwa tunatoka huko tulipata ajali mbaya sana gari tulilosafiria lilipondeka lote na watu wakajua tumekufa...nilikaa miezi tisa nikijiuguza," anasema.

Anasema baada ya kupona alifanya onyesho kubwa Kinshasa na baadae kuja Paris kwa mapumziko. Amesema kwa sasa anaandaa albamu yake ya pili iitwayo "FOUDRE ".

**Je, nini kitatokea leo akiitwa na Papy Tex na Dilu Dilomona? Kwanini Empire Bakuba hiyo haisikiki? Haifanyi maonyesho? Kwanini aliaminiwa na Pepe Kalle? Aliingiaje Empire Bakuba? Empire Bakuba walikuja mara nyingi Tanzania, athari zake zilikuwaje Kongo, majibu ya maswali haya utayapata hapa.**



## Kona ya **Urembo**

Na Hidaya Machuppa



# Namna ya kutunza ngozi majira ya baridi







HALI ya hewa ya baridi, pamoja na unyevu wake wa chini, huharibu ngozi yetu, na kuifanya kuwa kavu na kutetemeka. Sio tu kavu lakini inapokanzwa ndani ya nyumba hupunguza zaidi ngozi ya unyevu.

Afya ya ngozi ni muhimu si tu kwa ajili ya kuonekana, lakini muhimu zaidi kwa sababu ngozi hufanya kazi nyingi muhimu za mwili. Miongoni mwa mambo mengine, inalinda mwili kutoka kwa virusi na bakteria nyingi ambazo mtu hupatikana kila siku. Pia hulinda dhidi ya miale ya jua ya hatari ya ultraviolet ambayo inaweza kuharibu seli. Ngozi yenye afya pia husaidia mtu kuguswa vyema na mabadiliko muhimu karibu naye kwa kuhisi maumivu au shinikizo. Miezi ya hali ya hewa ya baridi inaweza kuhatarisha sana afya ya ngozi, na kusababisha hali kama vile xerosis (ngozi kavu) au eczema (kuwasha, kavu, mabaka mekundu au vidonda kwenye ngozi) ambayo inaweza kutofautiana kwa ukali.

**VIGEZO VYA KUZINGATIA ILI KUTUNZA NGOZI YAKO.**

Paka mafuta kila siku. Mafuta ya petroli au cream-ni bora kuliko lotion kwa ngozi ya kawaida na kavu. Ikiwa una ngozi nyeti, chagua moisturizer bila harufu au lanolin. Paka moisturizer moja kwa moja kwenye ngozi yako yenye unyevunyevu baada ya kuoga ili moisturizer iweze kusaidia kunasa unyevu kwenye uso.

Osha ngozi yako, lakini usiiongezee. Utakaso mwingi huondoa unyevu wa asili wa ngozi. Inatosha kuosha uso wako, mikono, miguu, na kati ya mikunjo ya ngozi yako mara moja kwa siku. Ingawa unaweza suuza shina, mikono, na miguu yako kila siku, si lazima kutumia sabuni au kisafishaji kwenye maeneo haya kila siku.

Punguza matumizi ya maji ya moto na sabuni. Ikiwa una "kuwashwa wakati wa msimu wa baridi," pata mvua fupi za vuguvugu au bafu na kisafishaji kisichokuwasha, kisicho na sabuni. Mara baada ya hapo, weka cream nene au moisturizer ya aina ya petroli-jelly. Osha ngozi kwa upole.

Kuwa katika hali ya unyevunyevu. Hewa kavu inaweza kuvuta unyevu kutoka kwa ngozi yako. Humidifiers ya chumba inaweza kuwa na manufaa sana. Hata hivyo, hakikisha kusafisha kitengo na kubadilisha maji kulingana na maelekezo ya mtengenezaji ili kupunguza mold na fungi.

Jikinge na upepo. Funika uso wako na utumie mafuta ya midomo yenye mafuta ya petroli. Vilinda ngozi ambavyo ni pamoja na mafuta ya petroli na krimu zilizo na keramidi zinafaa pia.

Epuka baridi kali. Joto la baridi linaweza kusababisha matatizo ya ngozi au baridi kwa baadhi ya watu. Tazama daktari mara moja ikiwa unapata mabadiliko ya rangi katika mikono au miguu yako ikifuatana na maumivu au vidonda. Ikiwa unapata maumivu makali ikifuatiwa na kupoteza hisia kwenye kidole au kidole, unaweza kuwa na baridi.

Kinga ngozi yako kutokana na jua. Kumbuka kwamba jua la majira ya baridi pia linaweza kuwa hatari kwa ngozi. Hata wakati wa majira ya baridi kali, unapaswa kutumia kinga ya jua yenye kipengele cha ulinzi wa jua cha 15 au zaidi ikiwa unapanga kuwa nje kwa muda mrefu. Mfiduo mwingi wa jua unaweza kusababisha kuzeeka mapema kwa ngozi na saratani ya ngozi.




## Macho **Manne**

Na Paul Mng'ong'o 0676055444 email:mg'ong'opaul@yahoo.com

KWA mtazamo wangu mimi, uongozi wa Simba umefanya jambo sahihi kabisa kuachana na kocha mkuu na kocha wa utimamu wa mwili. Nasema haya bila kuwavunjia heshima kabisa wala kubeza uwezo wao. Lakini ukweli ni kwamba timu ilishaanza kupoteza shape na compatibility, timu ilishatoka kwenye falsafa yake na hakukuwa kunaonekana kama kuna mabadiliko yoyote ya timu hata baada ya watu kuheshimu matokeo yake (Robertinho) kwa muda mrefu wakiwa hawaridhishwi na uchezaji wa timu.

Simba ilikuwa inashinda kwa maamuzi ya uwezo wa mchezaji mmojammoja tu, lakini kama timu, ilikuwa mbovu kabisa siku nyingi na ilikuwa inafungika kirahisi sana. Jambo lingine ni kuwa mchezaji wa Simba akishuka kiwango, anakuwa ameshashuka, mwalimu hakuwa na uwezo wa kuinua viwango vya wachezaji. Kitu kingine ni kuwa, timu ni kama ilikuwa inaenda kishkaji sana na hakuna hali ya kujituma na kuvuja jasho uwanjani, morali ilikuwa chini sana ni kama vile intensity ya timu ilikuwa chini. Simba haikuwa timu inayotisha tena ilikuwa timu ya kawaida ambayo haina outstanding performance. Haya yote niliyoyasema ni kazi ya benchi la ufundi. So ilikuwa lazima awajibike sababu timu haikuwa inapanda bali inashuka.

Kwa upande mwingine, pamoja na hayo kwenye benchi la ufundi, bado kuna mambo mengi ambayo viongozi wa Simba wanatakiwa kujitafakari na kufanya mabadiliko kwenye mifumo yao ya kimenejimenti ili kuleta matokeo ya kudumu ndani ya klabu. Hii ni pamoja na kuleta tabia za ki-mpira zaidi kuliko kujivunia mifumo ya kitaasisi pekee. Simba wamefanikiwa sana kujenga mifumo ya kitaasisi kwenye klabu kiasi kwamba sasa hivi ukiangalia unaiona sura ya taasisi ndani ya Simba na si sura ya zamani isiyokuwa rasmi (Uholela). Hapa hatuwezi kudharau hata kidogo jitihada kubwa iliyofanywa na mwekezaji wa klabu hiyo, Bilionea Mohamed Gulam Dewji, maarufu kama Mo. Simba sasa hivi ina sura ya kitaasisi sana, jambo ambalo linavutia sana mazingira ya kibiashara na kuaminika zaidi, Pia Simba imejenga "Brand" Imara Afrika ambapo leo Ukisikia Simba unajua kabisa ni taasisi kubwa yenye heshima barani Afrika. Pamoja na hali ya sasa lakini mashabiki na wanachama wa Simba watakuwa na mtazamo mdogo sana kama hawatathamini hatua hii ambayo haikuwepo kabisa Afrika Mashariki. Hali hiyo niliyoielezea ndiyo imeletwa matokeo ya wazi na heshima kubwa kwa klabu ya Simba na Nchi kwa ujumla.



Lakini pia bila kuharibu umuhimu wa mafanikio haya ndani ya Simba, ni muhimu kujua kuwa taasisi za mpira zinahitaji zaidi mifumo ya ki-mpira. Ninapoongelea mifumo ya ki-mpira ninamaanisha ushiriki wa moja kwa moja wa uongozi kwenye mambo ya mpira ikiwa ni pamoja na kuwatumia watu wa mpira wenye mapenzi makubwa na timu hiyo. Watu wengi wanaofit kwenye mifumo ya kitaasisi si watu wa mpira na wanaofit kwenye mifumo ya ki-mpira mara nyingi hawafit kwenye mifumo ya kitaasisi. Sina hakika kama kuna ushirikishwaji wa dhati wa watu wa mpira kama kina Kibadeni, Kiwelo, kina Mustapha Hoza, kina Dalali, Mgunda, Matola na wengine wengi wanaofanana na hao. Kwa mtazamo wangu, hawa ni hazina kubwa ambayo Simba wanayo lakini haitumiki kikamilifu hasa mapema wanapoandaa mechi muhimu za ndani na za kimataifa. Hawa wangeweza kujenga hamasa kwa wachezaji, mbinu, spiriti ya upambanaji na hata panapohitaji mbinu za ligi yetu na utamaduni wake hawa wangefaa zaidi kuliko maafisa wanaofit ofisini ambao mbinu na "uhuni kwa maana ya ujanja" wa ki-mpira hawauwezi.

Sasa mifumo ya ki-mpira ikizingatiwa vyema na kukawa na mifumo ya kitaasisi, hapo ndiyo unapata matokeo ya kudumu na timu kuitwa klabu kubwa. Kwa mtazamo wangu, Yanga hawana mifumo imara sana ya kitaasisi kama Simba, ila wako vizuri sana kwenye mifumo ya ki-mpira ambayo kimsingi ndiyo mifumo yenye athari chanya za moja kwa moja uwanjani tofauti na mifumo ya kitaasisi ambayo kitaalam inaitwa "Supporting Systems" yaani mifumo saidizi.


# Wachezaji bora wa muda wote



**Na Valensi Mbaga**

MPIRA wa miguu ndio mchezo maarufu zaidi ulimwenguni unaofuatiliwa na unaochezwa zaidi ulimwenguni. Kwa hivyo, mpira wa miguu wa kisasa ni wa ushindani sana na katika historia yake, huku ukiibua vipaji vikubwa ambavyo vitakumbukwa siku zote.

Ni tabia ya kawaida ya wapenda soka wengi kulinganisha ubora wa wachezaji mbalimbali na wanaendelea kujadiliana kuhusu mchezaji bora wa soka wa wakati wote. Ingawa kwa kweli ni vigumu kulinganisha wachezaji tofauti kutoka enzi tofauti kutokana na jinsi michezo ilivyobadilika na kubadilika kwa miaka mingi, tutajaribu kutenda haki kwa wachezaji wote ambao wanakumbukwa zaidi katika historia ya soka na bado ukubwa wao unaishi kwa majina namafanikio yao.




### 10. ANDRES INIESTA

Sawa na Zinedine Zidane, Andres Iniesta ndiye kiungo mwenye ushawishi mkubwa katika kizazi chake na alikuwa mmoja wa nguzo za mafanikio kwa Barcelona na timu ya Uhispania ambayo ilishinda na kutawala ulimwengu wote. Iniesta alipitia akademi ya Barcelona maarufu ya La Masia na akaingia kwenye kikosi cha kwanza.

Alikuwa na kipaji kama mchezaji wa akiba aliyechelewa na aliisaidia Barcelona katika mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa wa 2006 dhidi ya Arsenal. Iniesta alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mechi katika fainali za 2009 na 2015 za Ligi ya Mabingwa kwa Barcelona na alikuwa mchezaji mzuri wa mchezo.

Ingawa hakuwahi kuwa na ustadi wa kufunga mabao mengi na mara zote alikuwa msanii na muundaji katika safu ya kiungo, Iniesta alifunga bao ambalo liliipa Hispania Kombe lao la kwanza la Dunia nchini Afrika Kusini mwaka 2010. Iniesta aliondoka Barcelona mwaka 2018 akiwa na historia isiyo na kifani. pengine ni mchezaji wa Kihispania mwenye kipawa zaidi kucheza mchezo huo na anajionea awamu ya mwisho ya maisha yake akiwa na Vissel Kobe ya Japan.



### 9. ZINEDINE ZIDANE

Zinedine Zidane anachukuliwa kuwa mmoja wa viungo wa ajabu wa kizazi cha kisasa. Zidane alikuwa na kazi nzuri akiwa na Juventus nchini Italia lakini alikuja kujulikana kwa mara ya kwanza na ulimwengu kufuatia uchezaji wake mzuri wakati wa Kombe la Dunia la 1998 lililoandaliwa nchini Ufaransa.

Kiungo mshambuliaji aliiongoza timu hiyo ya Ufaransa kutoka mbele na alikuwa na msimamo katika muda wote wa mashindano. Alifunga mabao mawili ya vichwa kwenye fainali dhidi ya Brazil ya Ronaldo na ikaonekana kuwa tofauti wakati Ufaransa ilishinda Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza katika historia yao. Zidane alifuata mafanikio hayo kwa ushindi katika michuano ya Ulaya ya 2000 na kutawazwa mchezaji bora wa michuano hiyo.

Zidane baadaye alihamia Real Madrid ambako angepata umaarufu na mafanikio zaidi na alifunga volley maarufu duniani akiwa nje ya eneo la hatari dhidi ya Bayer Leverkusen ambayo iliisaidia Los Blancos kushinda UEFA Champions League mwaka wa 2002. Alistaafu mchezo huo mwaka wa 2006 lakini baadaye. alikuwa na kazi nzuri ya ukocha, akiiongoza Real Madrid kushinda mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa kati ya 2016 na 2018.

### 8. RONALDO NAZARIO

Ukweli kwamba Ronaldo Nazario alichezea Barcelona, Real Madrid, Inter Milan, na AC Milan na bado hakupata aina yoyote ya chuki ni uthibitisho wa kipaji na utu aliokuwa nao kwenye medani ya soka ,Kwa jina la utani 'O Fenomeno' au la kushangaza, alikuwa rahisi kutambuakwamba Ronaldo angepanda juu ya soka la dunia na kutawala mchezo mapema kabisa.

Alichukua soka la Ulaya kwa dhoruba katika PSV Eindhoven na alikuwa na msimu wa kuvunja rekodi na Barcelona. Baadaye alihamia Inter Milan na alikuwa nyota wa Kombe la Dunia la 1998 na 2002, ambalo angeshinda na Brazil kama mchezaji bora wa mashindano!

Ronaldo alishinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka 1997 na 2002 na uwezo wake kama mshambuliaji ulikuwa wa kipekee na kumfanya aonekane bora. Kama si majeraha, Ronaldo angekuwa na kazi ndefu na yenye mafanikio zaidi na pengine angeshika nafasi ya juu zaidi kwenye orodha hii.

### 7.FRANZ BECKENBAUER

Franz Beckenbauer daima atakuwa kielelezo cha beki bora na anachukuliwa kuwa beki bora zaidi katika historia ya soka. Beckenbauer alikuwa amebadilisha nafasi ya kucheza zaidi miaka ya 1960 na 1970 akiwa na Bayern Munich na Ujerumani Magharibi na pia alisonga mbele na kuchangia pakubwa mashambulizi ya timu yake.

Beckenbauer alijulikana kwa upendo kama 'Der Kaiser' au Mfalme kwa sababu ya mtindo wake wa kifahari, utawala na uongozi. Mjerumani huyo pia ni mmoja wa wachezaji tisa pekee walioshinda Kombe la Dunia la FIFA, Ligi ya Mabingwa ya UEFA pamoja na Ballon d'Or.



Beckenbauer alishinda ubingwa wa Ulaya mara tatu mfululizo akiwa na Bayern Munich kati ya 1974 na 1976 na pia alinyanyua Kombe la Dunia la FIFA la 1974 akiwa na Ujerumani.

Der Kaiser alierudia kazi hiyo kwa mara nyingine tena kama kocha mkuu wa Ujerumani mwaka 1990 na ni mmoja wa watu watatu mbali na Mario Zagallo na Didier Deschamps walioshinda Kombe la Dunia kama mchezaji na kocha.

### 6.ALFREDO DI STEFANO

Enzi za kabla ya Pele ilitawaliwa zaidi na Alfredo Di Stefano. Anachukuliwa kuwa mchezaji bora katika historia ya Real Madrid na kipaji cha Di Stefano kilifungua njia ya mafanikio zaidi kufuata huko Los Blancos.

>> INAENDELEA UK. 23

# Wachezaji bora  wa muda wote

>> INATOKA UK. 22

Fowadi huyo wa Argentina, aliyepewa jina la utani la ‘The Blonde Arrow’ alitawala kabisa hali ya soka katika miaka ya 1950 na alikuwa na maisha marefu ya miaka 20 ambapo alikuwa kinara wa mchezo .Di Stefano anajulikana sana kwa mafanikio yake akiwa na Real Madrid na alishinda

Mashindano matano mfululizo ya Europa akiwa na klabu hiyo na kushinda tuzo nyingine 15.

Di Stefano aliunda ushirikiano wa kutisha na wachezaji wengine maarufu kama Paco Gento na Ferenc Puskas na atakumbukwa kwa uchezaji wake katika michezo mikubwa. Anashikilia rekodi ya kufunga katika fainali tano za Kombe la Ulaya na ndiye mchezaji pekee aliyefikia kiwango hicho.

Pamoja na Maradona na Messi, Di Stefano anachukuliwa kuwa mfano wa kandanda nchini

Argentina ingawa hakuwahi kucheza Kombe la Dunia.



**5.JOHAN CRUYFF**

Tumejadili wachezaji wengi wazuri hadi sasa, lakini hakuna mtu mmoja ambaye amekuwa na athari kubwa kwenye historia ya mchezo na viwango vya mchezo wa kisasa kama Johan Cruyff.

Alikuwa tu gwiji wa soka na mwanafikra mkuu wa mchezo ambaye alileta falsafa ya ‘Total Football’ kwa Ajax, Barcelona, na kwa Timu ya Taifa ya Uholanzi.

Alikuwa mwanasoka wa kwanza kushinda Ballon d’Or mara tatu na Cruyff alitwaa Europa akiwa na Ajax, akishinda Mashindano matatu ya Uropa na kisha kutawala Uhispania akiwa na Barcelona. Aliwaongoza wababe hao wa Catalan kunyakua taji lao la kwanza la ligi katika kipindi cha miaka 14 na kuwabadilisha na kuwa vinara kwa mara nyingine tena.

Alikuwa pia kiongozi wa timu kubwa zaidi ya kandanda ambayo haikuwahi kushinda kombe la Dunia, upande wa Uholanzi wa 1974. Katika miaka yake ya baadaye, Cruyff aliweka jiwe la msingi la Barcelona ya kisasa na falsafa yake ya tiki-taka, akianzisha La Masia, kuanzishwa kwa rondos na makocha wenye ushawishi kama Pep Guardiola, Frank Rijkaar, Ronald Koeman, Louis Van Gaal, Xavi, Luis Enrique, Mikel Arteta, Ernesto Valverde, Marco Van Basten na Roberto Martinez miongoni mwa wengine.

**4.CRISTIANO RONALDO**

Cristiano Ronaldo amefafanua kizazi cha kisasa cha soka na ushindani wake na Lionel Messi ulipeleka mchezo kuwa na nyuso mpya. Ni mmoja kati ya wafungaji mahiri zaidi ambao wamewahi kuwaona katika mchezo huo na ustadi wake wa kufumania nyavu hauna kifani.

Cristiano alikuwa mvulana mwenye kipaji katika klabu ya Sporting mjini Lisbon kabla ya kuonesha uwezo wake wa kushinda ulimwengu akiwa Manchester United na chini ya ulezi wa Sir Alex Ferguson.

Ilikuwa kipindi chake akiwa na Real Madrid ambapo Cristiano angeendelea kuwa mnyama na alishinda mataji manne ya UEFA Champions League akiwa na klabu hiyo, ikiwa ni pamoja na kushinda matatu mfululizo! Ronaldo pia aliiongoza Ureno kutwaa taji la UEFA Euro mwaka 2016, likiwa ni la kwanza katika historia ya nchi hiyo.Nyota huyu ambae kwa sasa anakiwasha katika timu ya AL Nassir ya nchini Saudi Arabia bado amezidi kuwa bora na kuendelea kuonyesha kuwa anastahili kuwa katika nafassi hii.

**Pele ameshinda Kombe la Dunia mara nyingi zaidi kwa mchezaji katika historia, baada ya kunyakua taji la Jules Rimet mara tatu na ukweli huo pekee unatosha...**





**3.PELE**

Gwiji wa Brazil Pele alishikilia taji la kuwa mchezaji bora wa kandanda wa wakati wote na kwa maoni ya watu kadhaa, haswa wale mashabiki wa kizazi cha zamani, yeye bado ndiye mfalme.

Pele ameshinda Kombe la Dunia mara nyingi zaidi kwa mchezaji katika historia, baada ya kunyakua taji la Jules Rimet mara tatu na ukweli huo pekee unatosha kumweka kwenye mjadala.

Pele anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga katika Kombe la Dunia na hata alifunga mabao mawili katika fainali ya Kombe la Dunia la 1958 lililofanyika nchini Sweden. Ingawa alicheza mechi moja pekee katika Kombe la Dunia la 1962 ambalo Brazil pia ilishinda, Pele alithibitisha kilele chake cha kweli kwa ulimwengu wa kandanda mnamo 1970.

Alikuwa katikati ya timu ya Brazil yenye ujuzi na ya ajabu ambayo ilifanya haki kwa falsafa ya Jogo Bonito wakati wa Kombe la Dunia. Pia alikuwa na kazi ya kuvutia sana na New York Cosmos na Santos katika soka ya klabu. Pele atabaki kuwa kiwango cha dhahabu katika historia ya soka.

**2.DIEGO MARADONA**

Diego Maradona alikuwa zaidi ya mchezaji wa mpira wa miguu kwani alikuwa na uwezo wa kufanya mambo kwenye uwanja wa mpira ambao wanadamu wangeweza tu kuota. Akiwa na ustadi wa hali ya juu, Maradona alivutia watu wengi nchini Argentina kama kipaji cha hali ya juu na akajitengenezea historia katika Argentinos Juniors.

Alikua mchezaji ghali zaidi duniani wakati huo alipohamia Barcelona mwaka wa 1982 na kisha tena Napoli mwaka 1984. Ilikuwa na Napoli ambapo alifikia urefu mkubwa zaidi wa maisha yake ya klabu na aliongoza vazi la Italia ambalo wakati huo lilikuwa na matatizo kwenye Scudetto. kichwa.

Hata hivyo, athari kubwa ya Maradona kwenye soka ya dunia ilikuja na Argentina. Alichokifanya wakati wa Kombe la Dunia la FIFA la 1986 huko Mexico kinatosha kumweka juu kwenye orodha hii kama mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Maradona hakuzuilika huko Mexico na kipaji chake kitang'aa kila wakati katika mchezo wa kisasa.

**1.LIONEL MESSI**

Lionel Messi sio tu amekuwa mchezaji bora zaidi duniani kwa muongo mmoja na nusu uliopita, pia ni mmoja wa wanasoka bora zaidi wa wakati wote. Messi alikuwa tayari ameshinda kila kitu ili kushinda katika maisha yake ya klabu akiwa na Barcelona. Baada ya ushindi wa hivi majuzi wa Copa America na Kombe la Dunia la FIFA akiwa na Argentina, Messi ana sifa za kweli za kuwa mchezaji bora zaidi wa wakati wote.

Alianza kwa mara ya kwanza kwenye eneo la tukio akiwa kijana mwenye sura mpya katika Barcelona ya Frank Rijkaard na kumvutia kila mtu kwa kasi yake mbichi na uwezo wa kupiga chenga. Messi basi akawa mchezaji bora kabisa duniani chini ya Pep Guardiola na alikuwa uso wa timu hiyo ya Barcelona iliyotawala Ulaya.

Kwa kweli, ilikuwa wakati wa awamu hii ambapo alivutiwa kwa mara ya kwanza na kelele kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote. Katika muongo mmoja ujao, ameunganisha tu madai hayo kwa mafanikio yanayorudiwa na mfululizo na kwa sasa nyota huyo anakipiga katika klabu ya Inter Miami ameweza kubadilisha maisha yake ya awali na kwa upande wa kimataifa amekuwa akitisha akiwa na Argentina.

Ndiye mchezaji aliye na mataji mengi zaidi katika historia ya soka baada ya mchezaji mwenzake wa zamani Dani Alves na hakuna aliyeshinda Ballon d'Or zaidi ya saba ambazo Messi anazo kwa jina lake,Na kwa sasa Messi anazo nane.

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Novemba 08-14, 2023 |





# Sven kumrithi Mr. Objective

## • Yanga yamng'oa Robertinho

**Na Mwandishi Wetu**

SIMBA imeanza mazungumzo na kocha wake wa zamani Sven Vandenbroeck kwa ajili ya kurejea tena kuinoa timu hiyo katika mashindano mbalimbali.

Simba walianza vikao na Kocha huyo ambaye kwa sasa hana timu baada ya kuhitilafiana na uongozi wa klabu ya CR Belouizdad ya Algeria. Kipigo cha mabao 5-1 kutoka kwa Yanga kimechochea zaidi kurejea kwa mwalimu huyo ambaye aliipa mafinikio Simba.

Kipigo hicho kimesababisha Simba kumtimua Kocha wake Robert Oliveria 'Robertinho au Mr. Objective ambaye amefungashiwa virago rasmi jana akiwa na kocha wa viungo, Cornela Hategimana.

Katika taarifa ya jana Simba wamesema wamefikia makubaliano ya panden hizo mbili kuvunja mkataba huku timu ikiachwa chini ya Kocha wa makipa, Daniel Cadena huku Suleiman Matola akirejeshwa kumsaidia.

Awali kulikuwa na taarifa za Juma Mgunda kupewa kikosi hicho baada ya kuondolewa kwa Mr. Objective lakini uongozi ukatoa taarifa za Matola na Cadena kukabidhiwa timu,

Sven aliondoka Simba mwaka 2021 ikiwa ni siku moja tu baada ya kuivusha timu hiyo katika hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika. Sven alipata mafanikio mbalimbali akiwa Simba, ikiwemo ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA, Ngao ya Jamii.

Sven alifanya kazi na Matola kama Msaidizi wake, Mara baada kutoka Simba, kocha huyo alikwenda Saudi Arabia na baadae kuinoa Wydad Casablanca ya Morocco kabla ya kujiunga na CR ambayo siku chache zilizopita walivunja mkataba.

Kwa upande wake Robertinho katika mechi 17 alizoiongoza ameshindwa mechi moja dhidi ya Yanga lakini akiiwezesha kuingia hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.


Robertinho amekuwa akilalamikiwa kwa kikosi chake kutokutoa burudani bali imekuwa ikishinda kwa bahati. Simba ilihama kutoka kwenye mpira Samba Loketo mpaka mpira Kokoto. Sven ndiye muasisi wa pira Sambusa.

## Gamond: Tutashinda na madoido

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya Yanga, Migeul Gamond amesema kikosi chake kitaenda kutoa burudani na udambwiudambwi pamoja na kushinda mechi ili kutoa starehe.

Gamond amesema mchezo wa soka bila udambwiudambwi hauwezi kuwa mpira na hata ushindi bila ufundi kuonyeshwa uwanjani hakuleti maana halisi ya soka.



"Timu inapaswa kushinda, lakini inapaswa kutoa burudani uwanjani, hii inaleta starehe kwa mashabiki ambao wanatazama soka…tukishinda bila kutoa burudani haina maana," amesema kocha huyo.

Kocha huyo alisema katika ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Simba, ni matokeo ambayo yalimfurahisha mno na kwamba ni mechi ambayo ilimpa burudani kubwa kipindi cha pili.

Yanga imekuwa na kikosi kipana ambacho baadhi ya wachezaji ambao wameonekana kutoa udambwidambwi ni pamoja nakipa Djigul Diara, Max Nzengeli, Pacome Zouzou, Yao Kwasi, Skudu Makudubela, Joyce Lomalisa na Aziz Ki.

Safu hiyo imefanya Yanga sasa iitwe Pira Gamond ambapo timu hiyo mara nyingi kikosi hicho kimekuwa kikibadilika kushinda na kuanza kutoa udambwiudambwi.

Yanga leo wanacheza na ndugu wa Simba, Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga. Swali lililopo ni je, Coastal wanaoshika nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi wataweza kuwazuia mabingwa hao watetezi na kuwalipia ndugu zao kichapo?

Au tutashuhudia Kocha Fikiri Elias akiwafuata Mwinyi Zahera na Robertinho?

## Mmiliki Town Classsic, Rigo Star wafariki

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

MMILIKI wa bendi ya Town Classic inayoongozwa na Papii Kocha, Patrick Kessy amefariki dunia mjini Arusha baada ya kuugua ghafla.

Kaka wa Patrick, Rodgers Kessy alisema mdogo wake aliugua ghafla juzi na kukimbizwa hospitali ambapo alikata roho.

Rodgers alisema mwili wa Patrick ulitarajiwa kusafirishwa jana kutoka Arusha kupelekwa Dar es Salaam ambapo utaagwa nyumbani kwake Mbezi ambapo mazishi yake yatafanyika Ijumaa mkoani Kilimanjaro.



Patrick Kessy



Rigo Star

Wakati huohuo, mwanamuziki mahiri wa Kongo Rigo Bamundele maarufu kama Rigo Star amefariki dunia jijini Paris, Ufaransa.

Rigo ambaye alikuwa mpiga solo aliwahi kmuoa mwimbaji maarufu Afrika, Mbilia Bel mara tu baada ya ndoa yake na Tabu Ley kuvunjika.